


YULE MFARIJI

 Asante, Ndugu Neville. Asante, ndugu. Habari za jioni, marafiki. Ni majaliwa kurudi katika nyumba ya Bwana tena, usiku wa leo, katika huduma Yake, kumtumikia tena. Nafikiri ndilo jambo kuu sana lililopata kunifanyikia, kuwa na majaliwa ya kumtumikia Yeye. Nami najua, ninapowatumikia nyinyi, ninamtumikia Yeye. “Kwa kuwa kadiri mlivyomtendea aliye mdogo sana wa hawa, watoto Wangu, mmenitendea Mimi.” Na halafu Maneno Yake hayawezi kushindwa kamwe.

² Sasa ninataka kuchukua muda huu wa wakati kusema ya kwamba mama angali anapumua, ama alikuwa wakati nilipoondoka hospitalini muda mfupi uliopita. Na mara baada ya ibada ya ushirika usiku wa leo, mimi na mke wangu tutakesha usiku wa leo pamoja naye. Tunatoka kwenda ho—hospitalini.

³ Nami ninataka kuelezea kwa niaba yake, kwa kuwa hawezi, shukrani tulizo nazo kwenu nyinyi watu, kwa kutuomba katika wakati huu wa shida, na kwa kadi nzuri na maua, na vitu vya kuonyesha huruma, ambavyo mmentumia mama yangu; ambalo hakika ninalithamini, naye analithamini, pia. Na, asanteni, sana. Ningejaribu, kwa kadiri niwezavyo, kuwafanyia vivyo hivyo. Mnajua hilo. Na kwa hiyo tukijua jambo hili, kwamba labda . . .

⁴ Nisingeweza kusema ya kwamba yuafa, ingawa daktari anasema yuafa. Lakini aliniambia *hivyo*, Jumapili iliyopita, kwamba alikuwa yuafa wakati huo. Na juma zima, watoto wameketi karibu, wakingojea hospitalini, wakibadilishana zamu, saa baada ya saa, wakingojea mama aondoke. Lakini, wakati huu, yeye ni dhaifu kuliko alivyowahi kuwa.

⁵ Nafikiri daktari amepata kasoro ishirini na mbili kwake. Na ndipo basi kile wao, mwingine aliingia, akasema, “La, siamini ni hayo.”

⁶ Ndipo hatimaye, mmoja akasema hivi: “Ni mama mzee aliyedhoofika, amechoka mno hawezi kuishi muda mrefu zaidi.” Kwa hiyo, nafikiri hilo kwa namna fulani linalielezea. Hiyo ni kweli. Yeye ni mama wa watoto kumi, na nyakati zimekuwa ngumu kwake. Tumeishi maskini. Na mambo hayajakuwa kama—kama vile yangeweza kuwa, nadhani. Lakini, naye amechoka tu na amedhoofika, na anaenda Nyumbani.

⁷ Na ni kwa furaha, na kwa hii—hii Injili kuu ambayo nimehubiri, ambayo ninaiamini sasa. Haifanyi kazi tu wakati—wakati mambo ni sawa, hufanya kazi yakiwa mabaya, pia. Ndiyo Faraja yangu. Nayo . . . Siwezi kuamini ya kwamba mama yangu anaweza kufa kamwe, kwa sababu ana Uzima wa Milele, mnaona. “Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi.

Kila aishiye na kuniadini Mimi, hatakufa kamwe.” Sasa, Bwana wangu alisema Hilo, nami ninayashikilia Maneno hayo. Ingawa sote tunatembea katika bonde, ni wale. . . Kama mchungaji wetu wa thamani, alasiri ya leo, alivyoyatamka juu yake; saa hizi zenye uchovu, za kuchosha, za mwisho hapa duniani.

⁸ Bibi Fordyce, rafiki yetu mwingine, ambaye amelala moja kwa moja karibu naye, akifa, akiwa na ugonjwa wa moyo. Na mara nyingi, upande wa pili wa barabara, tumeleta, tumenunua mboga chache na kadhalika kutoka kwa huyo mama. Aliishi hapa nje nchini karibu na kwa Zurschmiede. Na bila kujua ilikuwa ni yeye, mpaka nilipomtazama vizuri, yeye ana umri wa miaka sabini na mitano ama sabini na sita. Naye alikuwa na dada zake wawili wakubwa mle ndani, kumtembelea. Basi alipoondoka, nilienda pale, akasema, “Wewe ni Ndugu Branham, yule mwinjilisti?”

Nami nikasema, “Naam, mama.”

Ndipo akaanza kulia. Akasema, “Mimi. . . hiyo ni. . . nilisikia huyo ni mama yako papo hapo karibu nami, pazia tu kati yetu.”

Nikasema, “Naam.”

Akasema, “Labda tutaondoka, sote wawili, wakati ule ule.”

⁹ Nikasema, “Bibi Fordyce, kuna swali moja ninalotaka kukuuliza, dada yangu, nimetembea kupitia maeneo yako kwenye nyaya hizo ndefu za umeme huko nje, na kukuona huko nje ukichimbachimba kwa jembe, na kufanya kazi kwa bidii; kisha ninakuona ukileta mboga zako na kuzichuuza kote mjini, na kurudi.” Nikasema, “Ambapo, umejipatia riziki ya haki; lakini je, unamjua Bwana wangu, kama Mwokozi wako?”

Akasema, “Ninamjua, kama Mwokozi wangu. Katika neema Yake ninatumainia,” akasema, “anipitisho katika bonde la uvuli wa mauti.”

¹⁰ Nikasema, “Mama huenda asiweze kutembea pamoja nawe kule chini, lakini Yeye ataweza.” Kwa hiyo, tukaomba. Naye akashikilia tu mkono wangu hata karibu inibidi kuuvuta niondoke, nitoke nje.

¹¹ Upande wa pili tu wa hicho chumba, Bibi Gaither papa hapa, mama mwingine mkongwe, akaenda kuwa pamoja na Bwana, saa chache tu zilizopita. Naye alikuwa amekatwa miguu yote miwili, kutokana na kisukari. Nami nimemjua tangu. . . Naye mumewe amelala pale juu, huku kiungo kimoja kimekatwa. Basi ulimwengu umejaa huzuni.

Usitamani utajiri wa ovyo wa ulimwengu huu,
Ambao huoza upesi sana,
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Hayatapita kamwe!

¹² Na mimi, miaka thelathini na mmoja nimesimama nyuma ya hili dawati hapa, na kote ulimwenguni, kama vile nimedai ulimwengu kuwa ndiyo mimbara yangu. Halafu, nimejaribu kuwapa watu Neno hili la Uzima wa Milele. Na ndicho kitu pekee kinachoweza kusaidia unapofikia mwisho wa safari. Basi kwa nini tutumainie kitu kingine chochote? Tungeweza kutumainia nini? Kama... Mama aliponiambia, hivi majuzi, kwamba alikuwa tayari kwenda, nami nikaenda nikazungumza naye.

Kama tu nilivyomfanyia Bibi Broy, mama mkwe wangu, yapata mwezi mmoja kabla hajaondoka, nilishuka nikaenda na kuzungumza naye. Hata hivyo, nilikuwa nimembatiza, na kadhalika.

Nami nilimbatiza mama yangu mwenyewe, miaka thelathini iliyopita, moja kwa moja chini ya mahali ninapoishi sasa, mtoni, katika Jina la Yesu Kristo.

¹³ Nilimbatiza baba yake mwenye umri wa karibu miaka mia moja, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, katika maji yenye matope. Ninaweza kumwona maskini jamaa huyo mwenye mikono iliyopooza, akinishika kwenye uso, na kunikumbatia, akiniangalia usoni. Nitakutana naye tena ng'ambo ya pili. Loo, naam. Naam.

Matumaini yangu hayajajengwa juu ya kitu kingine

Ila Damu ya Yesu pamoja na haki;

Wakati yote yanayoizunguka nafsi yangu yakitoweka,

Basi Yeye ndiye tumaini langu lote na ngome yangu.

Juu ya Kristo, ule Mwamba wenye imara, ninasimama;

Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

Usiku wa leo ni ushirika, niliahidi kuwa hapa.

¹⁴ Billy aliniambia leo ya kwamba wengi wameomba mahojiano. Nami nilitaka kuwapa; lakini nilimwomba kama angeyaacha wakati huu. Nina hakika mnaelewa.

¹⁵ Nami nimeshtuka kidogo. Mnajua jinsi ungeshtuka. Lakini, hata hivyo, ni—ninamwamini Bwana wangu, na neema Yake yatosha. Ndiyo yote ninayohitaji. Kwa hiyo, niombeeni, kwa kuwa ninahitaji maombi.

Basi Mungu na awabariki sana kila mmoja wenu!

Na utakapofika mwisho wa safari, ninatumaini ya kwamba kamwe hutajaribu kufanya hivyo bila kuzaliwa mara ya pili.

¹⁶ Nilikuwa nikiwazia, kama, Billy pale; niliishika mikono ya mama yake, mke wangu, alipokuwa anaaga dunia, milango michache tu chini ya mahali alipo mama sasa. Alipoangalia kule

ng'ambo, naye alikuwa na ujuzi wa kule kabla hajafa; msichana tu, umri wa miaka ishirini na miwili, mama ya watoto wawili. Naye akasema, "Billy, umezungumza habari Zake, umehubiri habari Zake, lakini," kasema, "mpenzi, hujui ni kitu gani. Jinsi ilivyo tukufu!" Tulikuwa ndio kwanza tumepata njia hii nzuri ya kale ya Injili wakati huo. Akasema, "Dumu Nayo, Billy. Dumu Nayo! Kamwe usiache. Inaleta faida katika saa hii."

Nami nikasema:

Nitakutana nawe kwenye ile asubuhi, karibu
na yale malango maangavu, yang'aayo,
Wakati huzuni zote zimetoweka;
Nitakuwa nimesimama karibu na lile lango,
wakati malango yatakapofunguliwa wazi,
Mwishoni mwa siku ndefu ya maisha yenye
uchovu.

Jambo ndilo hilo. Ninaamini hilo kwa yote yaliyo ndani yangu. Ninaamini hilo. Ninatumaini ya kwamba ninaweza kukutana na kila mmoja wenu, asubuhi hiyo.

Mtanijua asubuhi, kwa tabasamu nililo nalo.

Kama vile Ndugu Neville na hao wengine wasemavyo, katika ule wimbo:

Nitakutana nawe asubuhi, katika Mji ule
uliojengwa mraba.

Ni halisi tu iwezavyo kuwa!

¹⁷ Niliona, wakija, siku chache zilizopita, wakitoka hospitalini, kuna hema lililopigwa hapa chini kwenye—kwenye uwanja wa Reli wa Pennsylvania. Ni, kati ya, ninaamini, kati ya Barabara ya 9 na ya 10, hapa chini kutoka kwenye Spring, ukija, kuna bango (lililosema): "huduma ya karama." Simjui huyo ndugu. Sijui kama nimewahi kukutana naye. Lakini yeye ni ndugu, naye yuko hapa mjini, akifanya mkutano. Nami najua—najua maana ya kuingia katika mji, na labda mji wa ukubwa huu, na bila. . . mtu akijizuia. Simjui. Wala kamwe hajaniomba niseme jambo hili. Lakini na—naamini lingekuwa ni jambo zuri sana kama ninyi watu wote, mnaotaka mahali pa kwenda, kama mngeshuka mwende, mumsikie ndugu yetu akihubiri Injili. Hana budi kuwa mmoja wa watoto wa Kristo, la sivyo asingekuwa huko nje akipiga hema lake, katika hali hii ya hewa baridi, ya Septemba, akijaribu kumfanyia Bwana wetu jambo fulani. Kwa hiyo, juma hili, mtembeleeni ndugu yetu kule chini, na mumsikilize akihubiri.

Na, sasa, nafikiri hayo yalikuwa ndiyo matangazo yote, yale ambayo ilinibidi kuzungumzia.

¹⁸ Lakini bila shaka ninataka kusema jambo hili moja. Ninathamini msimamo wenu nyote. Katika hali ya hewa kama hii, na nyakati kama hizi; nanyi mnakuja kwenye maskini kanisa

hili dogo, na kukaa hapa. Ningefanya nini bila ninyi? Tungeweza kufanya nini bila mmoja kwa mwingine? Hii ndiyo saa ya kushikamana pamoja.

Loo, watakuja kutoka Mashariki na
Magharibi,
Watakuja kutoka nchi za mbali,

¹⁹ Nilitaka Meda na Mabel waniimbie huo asubuhi ya leo. Lakini, bila shaka, wasingeweza kufanya hivyo katika saa hii. Huo ndio wimbo walioniambia nilipoanza safari zangu za kiinjalisti, yapata miaka kumi na mitano iliyopita. Mmeusikia huo wimbo.

Kula pamoja na Mfalme wetu, kula kama
mgeni Wake;
Jinsi hawa wasafiri walivyobarikiwa!
Wakiutazama uso Wake uliotukuka
Unaowaka kwa upendo wa Kiungu;
Washiriki waliobarikiwa wa neema Yake,
Wataangaza kama vito katika taji Yake.

²⁰ Sasa, asubuhi ya leo ilinibidi kuharakisha kutoka. Nami . . . Mama alikuwa amepata afueni. Alikuwa karibu kusongwa roho. Karibu hakuwa akipumua, tena, waliponipigia simu. Lakini, kwa namna fulani, akapata afueni tena, akaanza kupumua tena. Yeye hajui. Lakini Yeye alimweka hai nilipokuwa nikihubiri, na kumweka kwa muda. Nami ninatumaini Yeye atafanya hivyo sasa wakati nikiwa hapa usiku wa leo. Sasa, asanteni sana, kwa maombi yenu.

²¹ Na sasa hebu na tuinamishe tu vichwa vyetu kwa muda kidogo tu tunapoomba. Huku tumeinamisha vichwa vyetu, na—nataka kuwaulizeni swali zito sana. Nami natumaini ya kwamba hamtachukizwa na mimi kuuliza hili; lakini nikijua, kama nijuavyo sasa, ninamaanisha hili kwa vijana na wazee. Ninyi wasichana wadogo, hamna budi kuja siku moja ambapo mama amelala usiku wa leo, ninyi vijana wanaume. Sisi sote tunajua ya kwamba hatuna budi kuja mahali hapo.

²² Na kama huna hakika kabisa ya kwamba uko tayari kukutana na Mungu, naomba uinue tu mikono yako, wakati hakuna mtu anayeangalia, kwa Mungu, na kusema, “Mungu, nikumbuke”? Mungu awabariki. Mungu awabariki, kila mahali. “Nikumbuke, Ee Mungu, sina budi kushuka kule ambako labda nitapoteza fahamu, pia. Lakini ninataka kuwa na hakika kabla sijaondoka, na wakati nikiwa na akili timamu, ya kwamba nafsi yangu imekusudiwa kwa Mungu. ‘Nami nitatembea kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya, kwa kuwa Wewe upo pamoja nami.’”

²³ Sasa, Baba wa Mbinguni, tunapoleta, kwa imani, mikononi mwangu, usiku wa leo, hawa watu wa thamani walioinua mikono yao sasa hivi. Ninawainua mbele ya Kiti cha Enzi cha neema

na rehema Zako. Huku nikijua jambo hili moja, Baba, huenda kukawa na wagonjwa hapa, huenda kukawa na watu wenye dhiki. Lakini, Mungu, hakuna hata mmoja wao aliye na haja kama hawa wanaoinua mikono yao. Kwa kuwa wanajua ya kwamba, haidhuru kama wameponywa maradhi, wataishi muda mrefu vya kutosha, labda watakuwa wagonjwa tena. Lakini, Ee Mungu, mara wanapomkubali Mwokozi huyu aliyebanikiwa na kuwa na Uzima wa Milele, na wamezaliwa mara ya pili, hakuna kitu, basi, kinachoweza kuwatenganisha na Mungu. Wanakuwa watoto wa Mungu, wala hawawezi kutenganishwa tena. “Amepita kutoka mautini kuingia Uzimani, wala hataingia hukumuni.” Ni ahadi ya jinsi gani, Bwana! Jinsi tunavyoweza kutia nanga nafsi yetu papo hapo! Haidhuru dhoruba inavuma kwa nguvu jinsi gani, haidhuru mawimbi yanaonekana kinyume vipi, “imani yetu inakutazama Wewe, Ewe Mwana-Kondoo wa Kalvari, Mwokozi wa Kiungu!” Sasa waingize usiku wa leo, Ee Bwana Mungu, katika rehema Zako na utunzaji. Okoa nafsi yao sasa hivi. Jalia wao—jalia wasiondoke kwenye jengo hili, usiku wa leo, mpaka hiyo “amani ipitayo ufahamu” iingie moyoni mwao. Nifanyeje, Bwana, baada ya wao kuinua mkono wao, ila kuinua sauti yangu Kwako, na kulia, “Ee Mungu, uturehemu”? Tujalie hili, Baba.

²⁴ Kwa kuwa katika miaka hii mingi ambayo Wewe umeniokoa, na kote kondeni na kote ulimwenguni, Nimewaona hao wakifikia mwisho wa safari, ambao hawakukujua Wewe, na kusikia hayo makelele ya kuomba rehema. Kisha nimewaona wale waliokujua wakija, wakiimba, “Siku ya furaha, siku ya furaha, tangu Yesu alipoosha dhambi zangu!” Loo, naam. Waovu huenea kama mti mbichi wa ghuba, mara nyingi; lakini anapofikia mwisho wa safari, ni tofauti.

²⁵ Jalia kusiwe na mtu mwovu miongoni mwetu usiku wa leo. Jalia wote wasamehewe kila dhambi. Na jalia kila mmoja humu ndani apokee usafi na upya kutoka kwa Mungu. Kwa kuwa, Baba, tuko tu kwenye mpaka sasa wa kufanya ushirika, agizo hilo takatifu, la dhati ambalo Wewe ulituchia. “Huu ni mwili Wangu uliovunjwa kwa ajili yenu. Hii ni Damu ya Agano Jipya, kikombe cha baraka. Kila muulapo na kukinywea, mwaitangaza mauti ya Bwana hata atakapokuja.”

²⁶ Mungu, tunaamini Wewe unakuja. Tunaamini ya kwamba Yesu atawasili, nasi tutamwona Yeye, Yule aliye mkuu mwenye utukufu. Ndipo uzee wote utapita, na ninii yote. . . huzuni zote na dhiki, na maradhi na kadhalika vitatoweka. Katika ile kesho kuu mpya, tutabubujika, Bwana, kwa vilio na shangwe za ushindi. “Tukitikisa mitende pamoja na hosana za furaha, kwa kuwa Mfalme atakichukua Kiti Chake cha Enzi.” Tunaitazamia saa hiyo.

Sasa tufariji sisi pia, Bwana, katika Neno Lako, usiku wa leo. Sema nasi mambo haya yanayostarehesha, yapate kuifariji

mioyo yetu.

²⁷ Nami ninamwomba mama. Bwana Mungu, yeye ndiye mama pekee niliyepata kumjua. Na kwa njia moja ama nyingine, haidhuru mke ni mwema jinsi gani, anaweza kuwa mwema kama wema uwezavyo kuwa, lakini haichukui mahali pa mama; mwaloni huo wa kale uliotandazwa, Bwana, uliokita mizizi na kuimarika, wakati unapoweza kushuka na kuketi karibu naye, na kuzungumza naye. Ninaomba, Mungu, ya kwamba Wewe hutamruhusu ateseke. Kwa kuwa linauvunja moyo wangu, Bwana, ninapowazia anateseka. Acha tu atembe katika bonde la uvuli wa mauti, bila kuogopa mabaya.

²⁸ Jinsi ninavyokushukuru! Muda mfupi uliopita, wakati hata hakujua jina lake mwenyewe, niliposema, “Yesu,” alitikisa kichwa chake, alimjua. Jinsi ninavyokushukuru kwa hilo, Bwana! Huku daktari akisema, “Amepoteza fahamu. Hajui chochote.” Lakini hata kama hakujua chochote, hata hivyo, yeye (ya hapa duniani), alikujua Wewe, Bwana. Nina furaha sana kwa hilo! Linaipa raha nafsi yangu.

²⁹ Hujasema na mtumishi Wako kuhusu kuondoka kwake. Si lazima unene nami, Bwana, kulihusu. Lakini laiti ningalijua, Bwana. Ninaomba ya kwamba Wewe utaninii tu... Chochote kile, Bwana, ninakikabidhi mikononi Mwako. Mapenzi Yako yafanyike.

³⁰ Na sasa, Baba, yabariki Maneno hayo usiku wa leo, Ujumbe, kusomwa kwa Neno, kuimbwa kwa nyimbo, kula ushirika. Yote na yawe kwa heshima na utukufu Wako, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Tunazo hapa lesa ambazo zinapaswa kuombewa. Nami nitaziendea baadaye kidogo, wakati tukiwa katika maombi.

³¹ Hebu na tufungue, usiku wa leo sasa, kwa ajili ya kusomwa kwa Neno. Nami nitajaribu kuharakisha niwezavyo, kwa sababu kuna wale wanaoketi, wakiningojea niende huko nje; na—na ni mchovu, nimedhoofika.

³² Ningetaka kuanza na mlango wa 14 wa Yohana Mtakatifu. Na hebu tuanzie kwenye—hebu tuanzie kwenye kifungu cha 12. Nalo somo langu usiku wa leo ni: *Yule Mfariji*. Na sasa tunaposoma, sikilizeni kwa makini hilo somo. Yohana Mtakatifu 14, kuanzia 12.

Amin, amin, nawaambia, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya; kwa kuwa mimi naenda kwa Baba.

Nanyi...mkiomba lolote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana.

Mkiniomba neno lolote kwa jina langu, nitalifanya.

Mkinipenda, mtazishika amri zangu.

Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele;

Ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui: lakini nyinyi mnamtambua; maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu.

Ningependa, kama mngeniwia radhi, nisome kifungu hiki cha 17 tena.

Ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, . . .

“Ulimwengu.” Mradi tu unaupenda ulimwengu, kamwe hutampokea. Unaona?

. . . kwa kuwa haumwoni, . . .

Haidhuru anafanya nini, ulimwengu haulioni. Hawaamini hilo. “Ni mhemko, saikolojia,” mnaona, kwao.

. . . haumwoni, wala haumtambui: . . .

Sasa sikilizeni, huyu “Yeye” anayenena juu yake:

. . . lakini mnamtambua; maana anakaa kwenu, . . .

Sasa, Yesu.

. . . na atakuwa ndani yenu.

³³ Hilo si ni dhahiri? Huyu Mfariji ni nani basi? Yesu. Mnaona? Alisema, “Nitamwomba Baba, atawatumia Mfariji mwingine, ndiye Roho wa Kweli; Ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumtambui, wala haumwoni, au, haumwoni, wala haumtambui. Lakini nyinyi mnamjua!” Mnaona, Yeye anazungunza juu yake Mwenyewe. “Mnamjua, kwa kuwa anakaa kwenu, katika mwili wa nyama sasa,” akizungumza na wanafunzi, “na atakuwa ndani yenu; na atakaa milele, asiondoke kamwe.”

³⁴ Loo, hivi Yeye si ni Mungu mwema? Yesu, ni mwema sana kwetu! Na imelezwa vizuri, kwamba, “Mungu wetu ni Mungu mwema.” Yeye ni mwema sana kwa watoto Wake! Ametuandalia kila kitu chema. Kila kitu tunachohitaji, Yeye amekiandaa. Kweli ungeweza kusema, “Baba yetu, uliye Mbinguni,” kwa sababu Yeye ni Baba. Na ingawa hatutii, ingawa tuna kibiri, Yeye angali anatupatia vivyo hivyo. Kama sisi ni wazuri ama kama sisi ni wabaya, Yeye hutupa chakula tule, nguo za kuvaa, nyumba ya kuishi. Loo, Yeye ni mwema sana!

³⁵ Laiti tungaliangalia huku na huku na kuhesabu mambo mazuri aliyo Yeye kwetu! Hatusimami kutafakari hayo. Vipi kama hukuwa na macho? Vipi kama hukuwa na pua, hukuwa na kinywa, hukuwa na masikio? Vipi kama hukuwa na miguu wala viungo, na usingeweza kutembea huku na huku? Lakini nyinyi. . . Lakini, mnaona, Yeye aliwapa miguu. Vipi kama hukuwa na macho wala usingeweza kuona; na, hata hivyo, ungeweza kusikia

kelele, bali hukujua zilikuwa ni nini? Sasa, zote ziko katika zile hisi tano ambazo Yeye hutoa.

³⁶ Lakini basi, kama tutaishi tu karibu Naye, Yeye atatupa kitu kingine. Huo ni ufahamu, kwamba tunaweza kuona kile mtu wa kawaida kamwe haoni. Tunapozaliwa mara ya pili, tunamwona Yeye. Mnaona? “Mnamjua Yeye. Mmemwona. Atakaa nanyi milele.” Loo, Yeye ni Baba mwema. Yeye ni—Yeye ni Chemchemi ya wema, chanzo kikuu cha wema wote na Ubaba ni wa Mungu wetu. Yeye ni mwema sana kwa watoto Wake waaminio! Lakini sasa labda . . .

³⁷ Kitu kimoja anachotuandalia, ni mwanga wa jua. Loo, jinsi ambavyo . . . Unajua, usingeweza kuishi bila mwanga wa jua. Usingeweza kuishi ila kwa muda mfupi tu, kwa sababu hakungekuwa na kitu kinachokua. Nao mwanga wa jua ni jambo kuu sana na unahitajika sana, hata hivyo tunaangalia tu na kusema, “Loo, ni jua,” na kuondoka. Mnaona, hatulitili maanani sana. Lakini mwanga huo wa jua ni muhimu kwa maisha yetu. Unatusaidia, na unatupa nguvu. Na, sasa, hiyo ni kwa mtu wa kawaida.

Halafu kuna mwanga wa kiroho wa Mwana ambao tunaweza kuishi ndani yake.

³⁸ Yote ya kawaida ni mifano ya kiroho. Kama vile tulivyokuwa na chakula kizuri tunachokula mezani, ni mfano wa Chakula kizuri tunachokula kutoka kwenye Neno. Mnaona, ni mfano tu. Ni dhihirisho la nje (sehemu ya kimwili) ya sehemu ya kiroho, ambayo inamaanisha zaidi kwetu kuliko hiyo sehemu ya mwili. Mnaona?

³⁹ Ni kama tu mtoto mchanga. Wakati mtoto mchanga amechukuliwa mimba katika tumbo la uzazi la mama, ni nyama tu na damu, ikirukaruka, ikitetemeka. Lakini, mara anapozaliwa, huioni, bali kuna roho na nafsi inayoning’inia karibu na mama huyo, ipate kuingia ndani ya mtoto huyo mchanga mara tu anapozaliwa. Mara tu mtoto huyo mchanga anapozaliwa, Mungu ameumba nafsi na kuumba roho, kuwa ndani ya mtoto huyo mchanga mara tu atakapozaliwa katika ulimwengu huu. Maskini mtoto huyo mchanga anakua na anaanza kujifunza, ndipo anakuwa nafsi hai na anajua mema na mabaya. Ndipo ananinii, kama tu vile Adamu na Hawa, walivyowekwa mbele ya mti wa mema na mabaya. Anafanya chaguo lake. Ndipo basi anakuwa na akili. Anakua wakati wote. Ni uchumi mkuu wa Mungu.

⁴⁰ Ndipo hatimaye anafikia mwisho wa safari, kwa ajili ya mwili huu wa kawaida. Na kama tu vile mwili huu unavyozidi kuzorota na kutoweka, kuna mmoja unaowekwa tayari kuupokea. Mara tu inapoondoka hapa, nafsi hii iliyo ndani yetu sasa na roho hii, inauacha mwili huu, na kwenda kwa mwingine; ulio mchanga, mzuri, ulio bora zaidi, ambao

hautazeeka, ambao hautapita. Mbona, Yeye ni Mungu mwema! Lakini, bila shaka ndivyo alivyo!

⁴¹ Lakini sasa, chukueni kwa mfano, vipi kama mtu anayejua kuhusu mwanga wa jua, nao unaangaza, halafu basi anakataa tu kuukubali mwanga huo wa jua? Akasema, “Kamwe siuamini huo.” Naye anashuka kwenye chumba chake cha chini, na kufunga mlango, na anakataa tu kujua jua linawaka. “Siamini hilo.”

Mtu fulani alisema, “Loo, kuna joto. Lina afya. Watu wanaoishi kwenye mwanga wa jua wana rangi, nao wana afya zaidi kama wanaishi kwenye huo mwanga wa jua.”

⁴² “Siamini hilo,” angesema, angejifungia tu ndani. Sasa, mtu huyo yuko katika hali ya kusikitisha. Kuna kasoro katika nguvu zake za akili, kama mtu akifanya hivyo.

⁴³ Na kama mtu atajifungia mwenyewe kutoka kwa mwanga wa kiroho wa Mwana wa Mungu, Kuna kasoro kwa hali yake ya kiroho, kwa kuwa, mtu anapokataa kutembea katika uongozi wa Mungu mwema, kama Mungu wetu, aliye Faraja yetu na Nguvu zetu. Na, kuishi katika mwanga wa Mwana Wake, ni kukua kiroho. Ni nguvu za kiroho kuishi katika mwanga wa Mwana Wake, kule kuangaza kwa Utukufu Wake! Mbona, ndiyo majaliwa makuu sana tuliyo nayo, kuishi chini ya mwanga wa Mwana wa Utukufu wa Mungu. Waangalie Wakristo wazuri, wenye afya!

⁴⁴ Mchukue mwanamume au mwanamke ambaye angejiweka chini kwenye chumba fulani cha faragha, na asingeona mwanga wa jua, mwanga wa jua la kawaida ambalo Mungu amempa, lakini anakataa kuamini hilo. Na, kwa sababu ya ubinafsi, anajifungia nje. Mtu huyo hivi karibuni atakuwa na upungufu wa damu, atapauka, hatakuwa na nguvu nzuri, hatakuwa na afya, naye hivi karibuni ataninii...kwa sababu amejiifungia mbali na majaliwa yenyewe ambayo Mungu alimpa. Hiyo ni kweli. Alifanya hivyo makusudi.

⁴⁵ Basi kama tukijifungia mbali na Utukufu wa Mungu, mbali na ubatizo wa Roho Mtakatifu, au ushirika wa Roho; muda si muda mwajua, tunakuwa Wakristo waliopauka, wagonjwa. Ujuzi wetu unazidi kuwa, hafifu. Basi yale majaribu makuu yajapo, tunasinyaa na kurudi nyuma.

⁴⁶ Inahitaji askari huyo ambaye ameishi katika Nuru ya Mwana wa Mungu, inahitaji roho huyo anayemjua Mungu, ambapo hapana wimbi la shaka; wanaweza kusimama katikati ya shida, na kupaza sauti, “Mkombozi wangu yu hai!” Haleluya! Jambo ndilo hilo, mnaona.

⁴⁷ Tunajifungia nje. Nao wanafanya hivyo, moja kwa moja, tunalifanya kwa sababu tunataka kulifanya. Lakini Mungu ni mwema, Yeye hutujalia hayo. Lakini wengi sana siku hizi hawataki kuingia mahali hapo penye afya pamoja na Mungu,

Mkristo mwenye afya, kuwa na roho yenye afya. Bila shaka ungejitahidi kupata mwili wenye afya, mtu yeyote angefanya hivyo. Vema, mwili huo, haidhuru unaweka afya kiasi gani katika mwili huo, unarudi mavumbini.

⁴⁸ Lakini, loo, ndugu yangu, nafsi hiyo haiwezi kuwa na afya kupita kiasi. Na kila wakati inapokua, inakua katika uweza na neema na nguvu za Mungu. Tunahitaji kutembea katika nuru ya Mwana wa Mungu, kwa sababu Yeye ni mwema.

Tuna urithi mkuu, dhamana kubwa takatifu ambayo tumepewa.

⁴⁹ Huenda ukashangaa sasa, “Ndugu Branham, unanena kuhusu mwanga wa Mwana, mwanga mkuu wa Mwana wa Utukufu wa Mungu, kufanya roho zenye afya, kutufanya Wakristo wenye nguvu?” Hilo ndilo lililotuleta hapa usiku wa leo, ni kutafuta kujua: “Tunapataje vitu hivyo? Vinatoka wapi? Ni nini? Nionyeshe ni nini, Ndugu Branham. Je, ninaweza kuvinunua kwenye duka la dawa? Ni vitamini ya aina gani?”

⁵⁰ Huvinunui kwenye duka la dawa. Lakini viko kwa wingi papo hapo karibu nawe, kama tu utavipokea. Ni kujua tu fomula, jinsi ya kuvipokea.

Kuna dawa katika duka la dawa, lakini hapana budi pawe na daktari wa kubaini ugonjwa huo. Kama hawakufanya hivyo, huenda ikakuua.

⁵¹ Kwa hiyo, basi, huna budi kuwa na ubaini wa huo ugonjwa. Huwezi tu kwenda na kumchukua mwenye dhambi na kumpa Roho Mtakatifu. Hana budi kutubu, kwanza. Hana budi kuoshwa, kuondolewa dhambi zake. Hana budi kujiandaa kwa ajili ya Vitamini hii kuu atakayopewa.

⁵² Sasa, tuna amana takatifu. Mnajua amana ni nini. Pia tuna urithi, urithi ambao tunarithi, kama watoto waaminio. Ni dhamana takatifu. Na dhamana hiyo takatifu na urithi wetu mtakatifu ni Neno la Mungu ambalo tumepewa, Neno kamili la Mungu. Neno Lenyewe ndilo Vitamini, Neno Lenyewe, Neno la Mungu!

⁵³ Hapo ndipo, sababu ya mimi kulazimisha kauli hivi, kama vile ningesema, kuhusu kusimama juu ya Neno hili! Haidhuru kitu kingine chochote kinasema nini, endapo hakiambatani na Neno, basi sikiamini; mnaona, ukitaka kukiamini, ni sawa. Lakini, kwangu mimi, inahitaji Neno, maana, “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa kamwe.” Kwa hiyo, inahitaji hilo Neno!

⁵⁴ Ninaishi kwa Neno. Yesu alisema, “Imeandikwa, ‘Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.’” Basi Hili Ndilo! Nalo Hilo tumepewa kama urithi. Ni urithi wetu, Neno!

Ee Mungu, jalia tuliwazie katika—katika kilindi Chake.

55 Ni—ni majaliwa yetu. Ni amana hii takatifu ambayo Mungu ameiweka kwa Kanisa Lake. Mungu alilipa Kanisa Lake Neno Lake. Na urithi huo mtakatifu ni wetu. Ni karama kutoka kwa Mungu. Sio tu kupatana juu ya *Hili*, na kukata *Hili*, na kutupa *Hili*, na kuongeza *hili* ndani, kukidhi ladha yetu wenyewe; bali kuhubiri Neno lote, Injili yote. Tunawajibika, kama Wakristo, kulichukua na kuliadini. Tunapojua, “Mioyo yetu isipotuhukumu, basi tunajua ya kwamba tuna kibali kwa Mungu.”

56 Lakini tunapojua tunakwepa Kitu fulani, kwamba baadhi ya ule urithi mkuu ambao ni wetu, kwamba tunaukwepa, kwa sababu kanisa letu lilisema wao “Hawaamini hili siku hizi, si kwa ajili yetu siku hizi.” Kama tukilikwepa Hilo, basi tunaharibu urithi wetu.

57 Sisi sote ni Wamarekani, nafikiri hivyo, ka—ka—kanisani usiku wa leo. Sisi sote ni raia wa Marekani. Tunashukuru kuwa Mmarekani. Lakini, hata hivyo, ilikuwaje kwa urithi wetu wa Marekani? Ilikuwa ni kitu gani? Tulianza kupatana. Na mara tunapopatana, tulipoteza utakatifu wa urithi wetu, kwa sababu tunapatana. Tuliwaacha marais waongoze zamu nne, hali linavunja ka—ka—katiba. Nasi tunafanya mambo siku hizi. Na sisi hata. . . Kwenye mita hii ndogo ya kuegeshea magari tuliyo nayo mtaani, hiyo ni kinyume na katiba. Hakuna kitu kama hicho kwenye katiba. Ni kinyume na katiba, hata hivyo tunakifanya. Na tunafanya kila namna ya mambo ambayo yanakiuka kanuni ambazo taifa hili liliwekewa msingi juu yake. Tunafanya kila kitu kinyume, kwa hiyo tunapoteza urithi wetu. Kwa sababu gani? Tulipatana juu ya kanuni ambazo liliwekewa msingi.

58 Mungu anisaidie, Mungu akusaidie, kama Wakristo, kamwe tusipatane kwa Neno moja la Neno la Mungu! Kwa kuwa amana hii takatifu ilikabidhiwa Kanisa, na ni jambo tukufu kuwa na Injili hii, Injili yote; kuihubiri, pasipo kupatana mahali popote. Ihubiri kama tu ilivyoandikwa. Iache kama tu ilivyoandikwa. Ni amana takatifu jinsi gani!

59 Na kama tukitarajia Neno hili kutimia kamwe, kama tukimtarajia Mungu kutimiza Neno Lake, hatuna budi kudumu Nalo jinsi tu Mungu alivyoliandika. Hiyo ndiyo sababu, kama mkikaa Nalo jinsi Mungu alivyoliandika, kutakuwa na mambo ya kila namna yakitendeka miongoni mwenu, kila Neno litatimizwa.

Niko chini ya matarajio sasa hivi, mimi mwenyewe, ya kuona nguvu zinazotikisa zikija, ambazo zitayatikisa mataifa hivi karibuni sana.

60 Mungu anaweza kuwaweka watu chini ya mamlaka Yake Mwenyewe, kama atampata mwanamume ama mwanamke ambaye hatapatana juu ya Neno Lake, bali atasimama pale

kama Mwamba wa Miaka, ambaye ataamini kila Neno Lake, na kuamini ya kwamba Yeye yuko nyuma Yake. Na mtu anayeliamini, huna budi kutenda kama Hilo. Kama hutendi kama Hilo, basi huliamini. Lakini, kama unaliamini, tenda kama Hilo! Nawe unaweza kulifanya litende kazi, nalo Neno litakuwa ndani yako.

⁶¹ Tulipoteza urithi wetu kwa sababu tu—tunapatana tu. Na tunapopatana, basi hatuwezi kutarajia kuninii... Mungu kutimiza ahadi Yake kwetu; kwa sababu tumevunja ile amana takatifu, na kuchafua amana ambayo Mungu alitupa. Na tudumishe amana hiyo; tudumishe ikiwa ya heshima sana, tudumishe ikiwa takatifu. Shikeni kila Neno Lake, wala msipatane popote. Mwaminini Mungu kwa Neno Lake, na mliamini. Tendeni kama Hilo! Simameni juu Yake! Msisogee! Hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya. Hicho ndicho Mungu anachotafuta.

⁶² Kama nilivyosema asubuhi ya leo katika ule Ujumbe, katika Ujumbe wetu asubuhi ya leo, nikinena juu ya, “Inatupasa,” ama, “Inatupasa kutimiza haki yote.” Ni juu yetu, ambao tumekabidhiwa Neno. Ni juu yetu, kwamba tudumu na Neno hilo. Na, tunapokaa Nalo, tunamwona Mungu akitenda kazi miongoni mwetu. Kwa hiyo, inatupasa, kudumu Nalo. Ni urithi ambao Mungu ametupa.

⁶³ Hebu na turudi nyuma kwa dakika chache tu, na tuwaone hao watu walioweka amana kuu, takatifu, ya Mungu. Hilo lilikuwa Neno Lake. Hilo ndilo tunalorithi, ni Neno. Na wakati wa shida, wakati wa mshangao, wakati wa dhiki, wakati wa nyakati za hatari, walipata faraja katika kulishika Neno.

⁶⁴ Neno ni Faraja ya Mungu. Unapojua, na unaweza kutembea chini hata kwenye bonde la uvuli wa mauti, na kujua ya kwamba Mungu alisema hivyo, hilo latosha. Mungu alisema hivyo!

Huwezi kusema, “Vema, mchungaji alisema hivyo,” ama, “Kanisa lilisema.”

⁶⁵ Unaweza kusema, “Mungu alisema hivyo!” Hiyo ndiyo faraja tunayopata. Hapo ndipo ninapoweza kupata faraja sasa. Hapo ndipo ulipopata faraja yako. Mungu alisema hivyo! “Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi, hatakuwa kamwe. Unasadiki haya?” Mnaona, ni faraja. Ndiyo faraja tunayopata.

Nuhu. Nilinena habari zake, ninaamini, asubuhi ya leo. Faraja ambayo hapana shaka aliipata, ingawa katikati ya ukosoaji! Bila shaka.

⁶⁶ “Kama ulimwengu hauwezi kumpokea,” Yesu alisema hivyo, “kwa sababu haumtambui. Lakini mnamtambua, na mmemwona. Naye anakaa kwenu, na atakuwa ndani yenu.”

⁶⁷ Nuhu alikuwa amekutana na Mungu. Alimsikia Mungu. Alikuwa na Neno la Mungu. Kwa hiyo haikuleta tofauti yoyote yale mtu mwingine yeyote aliyosema, Nuhu alikuwa na Neno la Mungu! Kwa hiyo, ilikuwa ni faraja kwake, wakati wakosoaji walipokuja, walikuwa wakiendelea na yale waliyokuwa wakifanya, wakimkosoa. Nayo sayansi, ikisema, “Maji yanawezaje kuanguka kutoka angani, wakati hakuna yoyote huko juu? Tunaweza kuthibitisha hakuna maji huko. Wewe ni mlokole, Nuhu! Mbona, ninaweza kukuthibitisha ya kwamba wewe ni mlokole. Angalia hapa, yako wapi maji yoyote? Nionyeshe!” Huenda walikuwa na darubini ambazo zingeweza kuona miaka milioni mia moja na ishirini ya anga la nuru, kama tulizo nazo siku hizi, ingawa unajua haikuwa imewahi kunyesha. Lakini hata hivyo, Nuhu alifarijika, kwa sababu alikuwa na ahadi ya Mungu. Amina.

⁶⁸ Alifanya nini? Aliendelea huku na huku akijenga safina. “Ujinga jinsi gani!” Huko, labda, kamwe hakujuwahi kuwako na mtumbwi. Hakukuwako na maziwa na mito, na kadhalika, katika siku hizo, kwa hiyo hawakuhitaji mtumbwi. Lakini, huyu hapa, akijenga kitu kinachoonekana kama kioja. Na kila mtu anamcheka. Na ilitosha kumvunja moyo; kila mpitaji, kasema, “Angalieni huko juu ya kilima, yule mlokole kule juu! Kile kitu anachojenga kama nyumba ni cha nini? Ni ki—kitu cha namna gani hicho? Halafu angalia anachokijengea! Mbona, ni upuuzi!” Lakini, hata hivyo, faraja aliyokuwa nayo Nuhu, kwa sababu alikuwa na Neno la Mungu! Ilikuwa ni faraja, alijua Mungu alisema hivyo. Amina. Mungu alisema jambo hilo, na hilo latosha. Mungu alisema hivyo!

“Unajuaje itanyesha?”

“Mungu alisema hivyo!”

“Unajuaje maji yatatoka huko juu?”

“Mungu alisema hivyo!” Hiyo ndiyo faraja aliyokuwa nayo, katika Neno.

⁶⁹ Hebu na tuangalie safina yake, kwa dakika chache, kwa namna fulani anaijenga kwa ulokole sana. Hivi mliona katika Mwanzo, Yeye alisema, “Ijenge kwa mvinje”? Sasa, kama uliwahi kuchukua na kuchunguza mti wa mvinje ulikuwa ni nini, karibu ni kama wa balsamu. Ni mti mwepesi sana, na ni kama tu sifongo. Wote umejaa masega madogo-madogo. Wakati ukiwa hai, ndani ya huo mti, una utomvu ndani yake. Na mara unapoukata, utomvu unamwagika. Kwa hiyo, hautengenezi kitu ila sifongo. Sasa Yeye alisema, “Usiijenge kwa mwaloni mzuri, mgumu. Usiijenge kwa mkuyu ama mbao ngumu; bali uijenge kwa mvinje, mti mwepesi kuliko yote na unaobonyea sana uwezao kuwepo.” Ukiwekwa ndani ya maji, ungezama katika dakika moja. “Ujenge kwa mvinje, na uutengeneze namna hiyo.”

Kasema inapaswa kuwa umbali gani na ya urefu gani, kisha kusema, “Weka vyumba ndani yake; vyumba vitatu.”

⁷⁰ Ni mfano mzuri jinsi gani: Kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu; vyumba vitatu. Mnaona? Basi kumbukeni, Yeye alisema, “Weka dirisha ndani yake.” Nalo dirisha halikuwa ubavuni; lilikuwa juu. Mnaona? Kuhesabiwa haki, Luther; utakaso, Wesley; ubatizo wa Roho Mtakatifu, ndipo Nuru inamulika ndani! Hiyo ni mwanga wa Mwana wa Mungu, ambao hatuna budi kuishi ndani yake, na kutembea katika Nuru. Basi kumbukeni, kwenye orofa ya chini, kulikuwa na vitu vitambaavyo; na katika orofa ya pili, walikuwako ndege; lakini juu kabisa kulikuwako Nuhu na familia yake, huko juu kusudi waweze kuona, ndipo nuru ikaingia.

⁷¹ Sasa Yeye alisema, ya kwamba, “Unapojenga hii kwa mvinje, ukiisha kuijenga yote na kuitengeneza, basi ninakutaka uitie lami, ndani na nje.”

⁷² Vema, nilikuwa nikisoma, siku moja, lami hii ilikuwa ni nini? *Lami*, kwetu, ni “rojorojo jeusi”; ambapo tunachukua kemikali na—na kutengeneza lami, na kutia lami barabara ka—katika nyufa, na kadhalika, kwa lami. Lakini, katika siku hizo, ilikuwa ni tofauti. Walikuwa na mti wenye ulimbo, nao wakachukua huu usiokauka na kuukata. Na badala ya—ya kuwa na vitu ambavyo sisi, kama tunavyofanya siku hizi, kutoa huo ulimbo, waliupigapiga huo mti. Nao wakaupiga huo mti mpaka utomvu na ulimbo ukatoka. Ndipo wangeupasha moto, na kuumwaga juu ya mvinje huu mwororo uliojaa . . . kama sifongo, nao ukajaa tu. Ndipo basi ulipokuwa mgumu, usingeweza kuupigilia msumari. Mnaona, ulikuwa tayari kupokea. Hiyo ni kama Kristo.

⁷³ Hilo ni Kanisa. Mnaona, Kanisa halina budi kujifanya tupu, na kupata nuru halisi, kuondoa umadhehebu wote kutoka kwako, kuondoa ulimwengu wote kutoka kwako, kuondoa kutokuamini kwote kutoka kwako, na kuondoka.

⁷⁴ Basi kulikuwa na Mwingine, ambaye alikuwa tofauti na sisi, ambaye alikatiliwa mbali katika maisha Yake ya ujana. Naye alichubuliwa na kupigwa, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu.” Alipigwa mpaka Uhai Wake ukamwagika, kama ulimbo kutoka kwenye mti.

⁷⁵ Na, loo, jinsi Mkristo anavyoweza kujilowesha Huo, loo, kama wewe ni mtupu. Lakini huna budi kujifanya tupu, kwanza. Shida yake ni kwamba, hatutaki kujifanya tupu. Lakini hebu na tuondoe, mawazo yetu yote, kanuni zetu zote za imani, vitabu vyetu vyote; na kujilowesha kwa Roho Mtakatifu, ambaye ni Mungu katika Neno Lake.

⁷⁶ Ndipo ungeweza kuabiri dhoruba, ungeweza kuabiri bahari, kwa sababu ulikuwa mgumu kuliko mti mwingine wowote. Hakuna kitu kingaliweza kuchukua mahali pake. Hakuna kitu kingeninii. . . Sehemu za safina zingali zipo; miaka elfu sita

iliyopita, nao wanapata sehemu zake, kwa sababu inadumu; kwa sababu ilifanywa ngumu sana, kutokana na kifuniko hiki kilichoizulia hukumu upande wa nje. Hayo maji yalikuwa ndiyo hukumu.

⁷⁷ Na tunapoingia katika Kristo, kupitia Maisha Yake yaliyopigwa, tumwingize ndani ya mfumo wetu. Tumechanjwa sana kutoka kwa mambo ya ulimwengu, hata wangeweza kuistahimili ghadhabu. Wakati dhoruba zinapiga na bahari ni ya mbisho, hata hivyo, maskini mtumbwi huo haushindwi. Unapenya moja kwa moja kupitia kwenye mawimbi, hadi kwenye Mwamba wa Miaka.

⁷⁸ Nuhu alikuwa na faraja, kwamba, alipokuwa akiijenga hii, alipokuwa akiitengeneza safina hii, alijua ya kwamba alifarijiwa, kwa sababu kwamba alikuwa na Neno la Bwana, lililomwambia, “Hayo ndiyo maagizo.”

⁷⁹ Vipi kama mtu fulani angalisema, “Aisee, Nuhu, unamaanisha nini kwa kujenga hiyo—hiyo kwa mvinje? Mbona, unajua ya kwamba mbao hizo, kama kungekuwako na maji, zingekuwa ndicho kitu cha kwanza kuzama.”

⁸⁰ Lakini, mnaona, Nuhu alikuwa akifuata maagizo. Alikuwa na Neno la Mungu, ambalo lilikuwa ni Mfariji Wake. Neno lilikuwa Faraja yake. “Sielewi ni kwa nini Mungu ananifanya niijenge namna hii, lakini *hivi* ndivyo alivyosema nifanye.”

⁸¹ Siwezi kuelewa ni kwa nini Mungu ananifanya nifanye jinsi nifanyavyo. Siwezi kuelewa ni kwa nini hataniruhusu nishirikiane na kufanya mambo haya mengine yote, na kuendelea na kanisa. Lakini *haya* ni maagizo Yake. Hivi ndivyo Yeye alivyosema ijengwe.

“Atafanya nini nayo?”

⁸² Sijui. Ninapaswa tu kuweka mbao kule juu, na kuzipigilia misumari. Na hizo Mbao ni Neno la Mungu. Na hiyo hapo faraja yangu, hiyo ni kweli, kwa sababu inajengwa jinsi Mungu alivyosema ijengwe. “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.” Hiyo ni kweli. Ni kitu gani? “Juu ya ufunuo wa kiroho kujua Yesu Kristo ni Nani.” Si nafsi ya tatu ya utatu; hakuna utatu ndani Yake. Yeye ni Mungu, na Mungu pekee, aliyedhihirishwa katika mwili. Hapo ndipo anapolijenga Kanisa Lake. “Na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.” Ingawa, ilionyesha malango ya kuzimu yangelipinga, bali kamwe yasingeweza kushinda.

Nuhu, hakika, Nuhu alikuwa na maneno haya. Alifarijika kwa sababu alijua, haidhuru ulimwengu ulisema nini!

⁸³ Vipi kama mkandarasi fulani angepitia hapo, na kusema, “Ndugu Nuhu! Unajua, kwa kuwa umeliacha kanisa na kuingia kwenye hamaki hii, hebu nikuonyeshe jambo fulani. Kama

unajenga, kwa nini usichukue mwaloni mzuri wa kale ulio imara?”

“Mwaloni hautafaa.”

Unasema, “Vema, ninaweza kuthibitisha ya kwamba mwaloni ni mti mgumu kuliko huu ulivyo.”

⁸⁴ Haileti tofauti yoyote jinsi mwaloni ulivyo mgumu; maelezo ya Mungu yalikuwa ni “mvinje.” Mungu atafanya jambo fulani na mbao hizo. Ana kitu cha kuongezea kwake.

⁸⁵ Baadhi yao husema, “Basi kwa nini usiende kwenye kanisa ambapo makundi makubwa ya watu wenye akili huja, waliovalia vizuri na nadhifu sana, na wanaoweza kukulipa vizuri, na mambo kama hayo; na kuihubiri Injili? Kwa nini unalihubiria kundi la watu maskini, hata nusura ufe kwa njaa, na kadhalika, na yote namna hii?” Wanasema hivyo kwa wahubiri wanaoitetea Kweli. Lakini, loo, ndugu, siwezi kukwambia! “Hivi hutachukua umati wa wasomi, mtu anayejua ABC zao?”

⁸⁶ Haileti tofauti yoyote ni umati wa aina gani. Wale walio tayari kumpokea Kristo, Kristo hufanya jambo fulani pamoja nao; ni—ni umati huo. Ni mtu huyo ambaye labda hajui ABC zake; lakini ikiwa hazijui, anamjua Kristo, na hiyo ndiyo tofauti. Mnaona, si—si—si—sio ule msimamo, ile damu ya samawati mnyodai kuwa nayo. Damu ya Yesu Kristo ndiyo—ndiyo inayotutia nanga na kutuweka salama ndani Yake.

⁸⁷ Hebu tumtaje tu mwingine, wakati tukiwa hapo. Ayubu, ninapenda kuzungumza juu ya Ayubu. Jinsi mtu huyo alivyokuwa na Mfariji! Mfariji wake alikuwa ni nani? Neno la Mungu! Mungu alimwambia ya kwamba ange—angekuwa mwenye haki, maadamu alitoa hiyo sadaka ya kuteketezwa. Ayubu alitulia kwa uchaji juu ya sadaka hiyo ya kuteketezwa. Haidhuru dhoruba zilipiga kwa nguvu jinsi gani, ni majipu mangapi yaliyotokea, ni vitu vingapi vilivyoondolewa kwake, angali alisimama kwenye Neno la Mungu. Lilikuwa ni Faraja kwa Ayubu.

⁸⁸ Wakati watu wake walipokuja, hayo makanisa, na kujaribu ku—kumpatanisha, na kusema, “Angalia hapa, Ayubu, angalia hapa, unajua ya kwamba umetenda dhambi. Unajua ya kwamba umefanya kosa. Mungu angemwadhibuje mtu mwenye haki namna hiyo, achukue yote aliyono nayo, awachukue watoto wake, aivuruge nyumba yake, afanye mambo haya yote, na kuiharibu afya yako? Nawe huyu hapa, umeketi hapa, mnyonge mwenye mashaka. Unafanyaje. . . Unawezaje kujihesabia haki, Ayubu, kwa kusema ya kwamba wewe ‘si mwenye dhambi?’”

⁸⁹ Lakini Ayubu alijua yeye hakuwa mwenye dhambi, kwa sababu alikuwa amesimama juu ya Neno! Amina. Mungu alihitaji hiyo sadaka ya kuteketezwa na ma—maungamo, naye Ayubu alikuwa ameungama na kusimama kwenye Neno. Naye alilia katikati ya matatizo yake, “Ninajua Mkombozi wangu yu

hai, Amina; katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi. Na ingawa mabuu ya ngozi yatauharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu.” Mnaona, faraja yake ilikuwa ni ahadi ya Mungu, Neno la Mungu.

Huo ndio urithi tulio nao, Neno la Mungu. Ni ahadi. Naam, bwana.

⁹⁰ Ibrahimu, tulizungumza juu yake asubuhi ya leo. Ningependa kumrudisha tena, usiku wa leo tu, kwa ajili ya ushuhuda mwingine. Ni faraja jinsi gani aliyokuwa nayo Ibrahimu, wakati huenda watu walimwita mlokole. Wakati kila kitu kilipomwenda mrama Ibrahimu, wangesema nini? “Unaenda wapi, Ibrahimu, pamoja na mvulana huyo mdogo?”

“Nakwea nikamtoe dhabihu.”

“Kwa nini?”

⁹¹ “Vema, kama Yeye ni Yehova, wakati aliponena nami; Mwenyezi Mungu, yule El Shadai, Kifua; nilipokuwa na umri wa miaka mia moja, naye mke wangu akiwa na tisini, Naye akanipa mtoto huyu; sasa, kama Mungu yuyo huyo anahitaji uhai wa mtoto huyu, nilimpokea kama mmoja kutoka kwa wafu, nina imani kwamba Mungu anaweza kumfufua kutoka kwa wafu.” Kwa nini? Hiyo ilikuwa ndiyo faraja yake.

⁹² Mnajua Ayubu alisema, katika wakati wake, “Ajaponiua, hata hivyo nitamtumainia.” Ametiwa nanga katika Neno. Alijua yale Neno liliyosema, na hiyo ilikuwa ndiyo faraja yake. Huo ulikuwa ndio msingi wake, kumpokea, kumshikilia.

⁹³ Naye Ibrahimu alijua ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu. Kwa hiyo kama mwanawe... Alikuwa amekufa, ninii yake... Tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekufa, uanaume wake ulikuwa umekufa, na hata hivyo Mungu alimpa mvulana huyu kwa sababu Yeye alimwahidi jambo hilo. Na kama Neno lile lile lililomwahidi hilo, lilimwambia “umtoe mwana kuwa dhabihu,” alijua ya kwamba Mungu aliweza kumfufua katika wafu.

⁹⁴ Sasa, ikiwa Mungu, aliyenifufua katika wafu, mimi mwenye dhambi, nimekufa katika dhambi na makosa; Yeye akaihuisha nafsi yangu; alinifanya jambo fulani; alikufanya jambo fulani; aliondoa roho hiyo ya ulimwengu kutoka kwangu; aliondoa shauku hiyo ya ulimwengu; aliniinua juu ya vivuli hivyo; kisha akanipa ubatizo wa Roho Mtakatifu; kama Mungu wangu anaweza kufanya hivyo, mauti hayawezi kunitenganisha Naye! La, bwana! Hakuna kitu kinachoweza kunitenganisha. Hiyo ndiyo faraja. “Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi.” Hiyo ni kweli! Najua! “Yeye aulaye huo mwili Wangu na kuinywa Damu Yangu, yuna Uzima wa milele, nami nitamfufua katika siku ya mwisho.”

⁹⁵ Kama Mungu angeweza kunichukua nilipokuwa chini katika matope na dhambi, na kuniinua, kunifanya Mkristo;

kama Mungu angeweza kunichukua wakati nilipokuwa nimefadhaika na kuhuzunika, na nilikuwa katika hali niliyokuwa, mnyonge mwenye mashaka, na kuniinua, kunipa tumaini la Uzima wa Milele, na kunibatiza kwa Roho Mtakatifu, na kunijaza nguvu na utukufu Wake; basi Yeye anaweza kunipitisha katika bonde la uvuli wa mauti, na kunipokea Utukufuni ng'ambo ya pili. Kwa sababu Yeye aliahidi jambo hilo, hiyo ndiyo faraja yetu.

Juu ya Kristo, Mwamba imara, ninasimama;
Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

⁹⁶ Wale wana wa Kiebrania, walipokuwa wakienda kwenye ile tanuru ya moto, kama tulivyozungumzia asubuhi ya leo, walipokuwa wakienda kwenye hiyo tanuru ya moto, kuyatoa maisha yao, walikuwa wamechukua msimamo wao, kama tulivyonena habari zake asubuhi ya leo. Lakini ni kitu gani kilichowapata? Walisema, "Mungu wetu anaweza." Amina. Papo hapo walisimama! Walisimama juu ya nini? Faraja yao ilikuwa nini? Katika dakika chache wangeteketezwa vipande-vipande. Tanuru ilitiwa moto mara saba kuliko ilivyowahi kutiwa moto. Lakini walikuwa na faraja! Kwa nini? Wakijua jambo hili, ya kwamba, "Mungu wetu anaweza kutuokoa na moto huo wenye hasira." Wao, faraja yao, ilikuwa ikitegemea uwezo wa Mungu waliyemtumikia. Loo, jamani!

⁹⁷ Wakitulia juu ya uwezo Wake! Hilo ndilo tumaini langu na ngome yangu. Ninatulia juu ya uwezo Wake. Ninatulia juu ya neema Yake. Si juu ya kile nilicho mimi; kile alichu Yeye. Ninatulia juu yaa ahadi Yake, kwa sababu Yeye alifanya hiyo ahadi na akaapa kwa hiyo ahadi. Nami ninajua ya kwamba tuna Uzima wa Milele. Hiyo ni kweli.

⁹⁸ Alitulia juu yaa hilo. Wale watoto wa Kiebrania walisema, "Yeye anaweza kutukomboza. Hata hivyo, asipofanya hivyo, kamwe hatutaisujudia sanamu yako." Ninapenda hilo. Naam, bwana.

⁹⁹ Ajaponikataa mwishoni mwa safari, Mkristo yeyote angeweza kusema, ingawa atanitupa katika utengano wa Milele, hata hivyo ninampenda, hata hivyo Yeye ni wangu. Katika kuzimu, ningali ninaweza kuwazia jinsi ninavyowazia sasa, ningali nitampenda. Nyakati zinapoendelea, ningali ninampenda; kwa sababu jambo fulani lilitukia moyoni mwangu, jambo fulani lilitukia. "Na kama ningalikuwa na maisha, au ningalikuwa na tatu; kama Bwana Yesu Kristo, ninatamani kuwa." Hiyo ni kweli, maana jambo fulani lilitukia. Yeye ni Uzima wangu. Alikuwa kwangu.

¹⁰⁰ Musa alijua. Wakati Musa alipokuwa na jukumu hilo la watu milioni mbili, wakati alipowaongoza kutoka Misri, atawalishaje? Watu milioni mbili, huku—huku wanawake wamebeba lundo la mikate iliyokandwa kichwani mwao, kwa miaka arobaini ya

safari, atawalishaje? Ni watoto wangapi wanaoweza kuzaliwa kila usiku, katika kundi la watu kama hao? Ni wangapi wazee na wagonjwa? Watachakaza nguo ngapi? “Nitazipata wapi hizo nguo? Nitawalishia wapi? Nimekuja kwao, kama kiongozi. Nitawezaje kufanya hivyo?”

¹⁰¹ Musa alitulia juu ya hili: maana, Mungu alisema, “Hakika nitakuwa pamoja nawe.” Hiyo ndiyo faraja yake, “Hakika nitakuwa pamoja nawe!” Hilo tu ndilo alilohitaji, kwamba, Musa alitulia juu ya faraja ya ahadi ya Mungu, “Hakika nitakuwa pamoja nawe, Musa.” Kwa hiyo, basi, si juu ya Musa kuona jinsi wanavyolishwa.

“Utafanyaje jambo hilo, Bwana?” Musa hakuuliza swali hilo.

¹⁰² Si kazi yangu kuuliza maswali. Si kazi yako kuuliza maswali. Ni kazi yetu kumwamini na kumtii, na kujisikia vizuri wakati tunapotulia juu ya ahadi Yake. “Mungu alisema hivyo. Hilo latosha.”

¹⁰³ Mtu fulani aliniambia wakati mmoja, “Ndugu Branham, hivi huogopi unapoenda mimbarani kule, na unaitwa kwenye mashindano ya kuamua? Hivi huogopi wakati mwingine, ukisimama kwenye mstari huo, kutakuwa na kosa?” La, bwana!

¹⁰⁴ Siogopi, kwa sababu ninatulia kwa uchaji juu ya Neno Lake: “Nitakuwa pamoja nawe,” aliponiambia usiku huo, “hakuna mtu atakayesimama mbele yako, siku zote za maisha yako,” alisema, “nitakuwa pamoja nawe.” Naye amekatilia mbali kila adui. Yeye amesimama pamoja nami wakati sikustahili kutetewa. Lakini, kwa sababu Yeye aliahidi hilo, kwa sababu ya neema Yake, nimetulia kwa uchaji juu ya Neno hilo. Kweli! Kwa sababu Yeye aliahidi hilo! Yeye aliahidi jambo hilo, Yeye anaweza kutimiza yale aliyoahidi. Hiyo ni kweli.

Musa alijua jambo hili. “Utavukaje bahari?”

Musa akasema, “Sijui, bali Yeye aliahidi ya kwamba atakuwa pamoja nami.”

¹⁰⁵ Kwa hiyo, kamwe usivuke daraja mpaka ulifikie. Dumu na Neno la Mungu, na Mungu ataifungua njia, kwa sababu Yeye ndiye Njia. Naam. Musa alifarijiwa na Neno ambalo Mungu alimwambia.

¹⁰⁶ Sasa, Yohana; ninaamini tulimrejea asubuhi ya leo, sina hakika, lakini na- . . . nadhani tulirejea kwa Yohana Mbatizaji. Huko nje nyikani, kama mtu fulani, alipokuja kwenye. . . Kasema, “Angalia hapa! Kuna zaidi ya watu milioni mbili katika Israeli siku hizi. Utamjuaje Masihi huyu? Utajuaje?”

“Atakuwa ni Mtu wa kawaida. Atakuwa mmoja wa wana wa Daudi.”

¹⁰⁷ “Yeye atapitia wapi, ukoo wa Daudi? Kuna maelfu mara maelfu yao. Utamjuaje? Utawezaje kumtambulisha kwa ulimwengu, na kujua kwamba ni Yeye?”

108 Akasema, “Ninalo Neno la Mungu. Nitamjua!” Akasema, “Kuna Mtu anayesimama katikati yenu sasa.” Amina. “Kuna Mtu anayesimama miongoni mweni sasa, Ambaye hamumjui. Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto.”

“Utamjua, Yohana?”

109 “Ninatulia juu ya Neno la Mungu. Kwa sababu Mungu, huko nyikani, aliyeniambia ‘Nenda ukabatize kwa maji,’ alisema, ‘Ambaye nitamwona Roho akishuka na kukaa juu Yake, huyo ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto.’”

110 Yohana alisema, “Alikuwa amesimama pale, bali mimi sikumjua. Alikuwa ni Mtu wa kawaida. Alikuwa amevalia kama mwanadamu, alionekana kama mwanadamu. Alikuwa Mwanadamu!” Kasema, “Sikumjua. Lakini Yule aliyeniambia huko nyikani. ‘Utaona ishara, na hiyo itakuwa ni Roho akitulia juu Yake. Yeye Ndiye atakayefanya jambo hilo.’” Yohana hakuogopa kwamba angefanya kosa; kwa sababu, alimjua Yeye! Amina.

111 Loo, tunawezaje kukosea, basi, wakati Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Kwa Jina Langu watatoa pepo, na kunena kwa lugha mpya; watashika nyoka au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; nao wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

112 Nao watu wa siku hizi wanaona ya kwamba wanakanusha mamlaka hiyo. “Wenye mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu za Roho Mtakatifu.” Hakika, limewekwa wazi tupate kuliona.

113 Tunafarijiwa, kwa sababu Neno la Mungu lilisema na kutuambia, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Alisema kutakuwako na wakosoaji watakaoinuka; wangesema mambo haya; kwa hiyo linapaswa kutufariji zaidi kwa ajili ya jambo hilo, kwa sababu tunalo Neno la Mungu, hiyo ni kweli, linalotwambia mambo haya.

114 Loo, naam. Yohana alimjua, kwa kuwa alikuwa na Neno la ahadi Yake. Mungu alimwahidi. Kasema, “Nitakutolea ahadi, Yohana. Utakuwa huko nje ukihubiri, endelea moja kwa moja na kuhubiri tu bila kujali matokeo. Wakati Mafarisayo na Masadukayo na madhehebu yote yanapokuja, usishirikiane nayo. Usiungane na yoyote yao, simama tu papo hapo na kuweka shoka kwenye shina la mti.”

115 Ndipo walipokuja, alisema, “Enyi uzao wa nyoka, ni nani aliyewaonya kuikimbia ghadhabu ijayo? Msianze kusema, ya kwamba, ‘tuna *hili* kwa dhehebu letu, tuna Ibrahimu ndiye baba yetu.’ Maana Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.”

Alifarijiwa, wakati wao, mtu fulani huenda alisema, “Ngoja kidogo. Huyu hapo kuhani mkuu upande ule mwingine.”

116 “Awe kuhani mkuu ama si kuhani mkuu, awe askofu ama si askofu, awe mfalme ama si mfalme”; yule pale Herode ameketi pale, naye Yohana akasema, “Si halali kwako kumchukua mke wa Filipino na kuishi naye.” Amina.

117 Alikuwa na nini? Neno la Mungu. Amina. Hakujali, alilithubiri bila kupatana. Yeye alikuwa na Neno; hiyo ilikuwa ndiyo Faraja yake. “Mungu aliniambia Masihi huyo atakuwa ni Nani.”

“Vema sasa, kama kutakuwako na Masihi yeyote, hivi hufikirii atakuwa kuhani wetu mkuu? Hivi hufikirii angejua habari zake?”

118 “Sijui kuhusu hilo. Lakini Mungu aliniambia, ‘Nitamwona Roho akishuka. Atakaa juu Yake. Yeye atakuwa Ndiye.’ Amina! Huyu atakuwa ndiye Masihi wangu.” Yohana akasema, “Nina faraja moyoni mwangu, inayongojea, kwa sababu ninajua ahadi ya Mungu. Nitakapomwona, nitamjua.”

119 Siku moja, hao hapo Lazaro na Yesu wakishuka chini ya kilima, wakishuka kilimani, wapate kuwa...Akaingia moja kwa moja majini.

120 Naye Yohana akasema, “Tazama, Huyu hapo! Huyu Ndiye!” Kila mtu aliangalia kote, wasingeweza kumtofautisha mmoja na mwenzake. Wote walifanana, wakiwa na ndevu zao na joho. Lakini Yohana akasema, “Ninamjua, kwa sababu kuna ishara inayomfuata. Ninamjua. Huyu Ndiye. Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu, aondoaye dhambi ya ulimwengu.”

121 Yesu kamwe hakuinua kichwa Chake, bali alienda moja kwa moja mtoni akabatizwe. “Hivi ndivyo itupasavyo kutimiza haki yote.” Alijua Yeye alikuwa ni Masihi, kwa sababu moyoni mwake alikuwa na Neno la Mungu na ahadi.

Loo, jinsi tunavyoweza kupumzika usiku wa leo!

122 Jinsi ambavyo wakati daktari anaondoka kitandani, na kusema, “Moyo huo unasambaratika tu. Mapigo hayo ya moyo yamekwisha. Kupumua kunashindwa. Yeye yuafa.”

123 “Lakini ninamjua Yule niliyemwamini, nami nime- . . . sadiki kabisa Yeye anaweza kukilinda kile nilichoweka amana Kwake hata siku ile.” Haleluya! Hakika, una ahadi ya Mungu, “Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi, hatakufa kamwe. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Tunayo ahadi, Neno la Mungu. Ni faraja kwetu, kudumu na Neno la Mungu.

124 Sasa hawa mashujaa wote mashuhuri, ambao nimeandika wengi wao hapa chini, lakini ili kuokoa wakati, tunajua ya kwamba walifarijiwa na Neno la Mungu. Haya hapa yale waliyofanya. Waliangalia nyuma, kama vile, mtu angeangalia nyuma na kuona ni vile, huyo mwingine alitimiza Neno akafarijiwa, kisha akatoka. Halafu basi *huyu* mwingine,

aliangalia nyuma na kuona yale *yeye* aliyofanya, kwa hiyo akalifuata Neno na kutoka; akafarijiwa, akijua alikuwa na ahadi ya Mungu. Mwingine akaja, akahisi Roho juu yake, na kujua; kwa hiyo akalifuata Neno la Mungu, akapata faraja aliyopata. Kila mmoja wao akilifuata Neno la Mungu! Hiyo ilikuwa ni faraja.

125 Loo, ndugu, sikiliza hili sasa: Siku moja Neno hilo lilifanyika mwili. Jambo ndilo hilo. Neno hilo lilifanyika mwili katika umbo la mwanadamu. Neno la Mungu, lililoleta faraja, lilifanyika Mtu hapa miongoni mwetu. Tungeweza kulishika Neno la Mungu mikononi mwetu. Tungeweza kupeana mikono na Neno la Mungu. Yeye alikuwa ni Neno. “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu.” Neno hilo la Mungu lilifanyika mwili, yule Mfariji. Aliishi hapa duniani. Tunaona ya kwamba Yeye alikuwa ni Neno. Alitenda kama Mungu. Alionekana kama Mungu. Alihubiri kama Mungu. Aliponya kama Mungu. Yeye alikuwa ni Mungu, kwa kila njia alikuwa ni Mungu! Alinena kama Neno. Alionekana kama Neno. Alihubiri kama Neno. Yeye alikuwa ni Neno! Amina.

126 Loo, ingekuwa ni faraja jinsi gani kuketi karibu Naye! Hivi hamngalipenda kufanya hivyo? Unasema, “Loo, hakika ningalipenda, Ndugu Branham.” Hebu kidogo. Mbona, ningemkimbilia, nikaketi karibu Naye, wakati alipokuwa hapa duniani!

127 Kamwe hapakuwapo na mtu ambaye angeweza kusimama kwenye ngozi ya kiatu Chake, angaliweza kusimama ardhini, na kusema, “Mimi ndimi Ufufuo na Uzima,” kwenye kaburi la Lazaro. “Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi.” Loo, jamani! Huyo alikuwa ni nani? Hilo lilikuwa ni nini? Hilo lilikuwa ni Neno. Yeye alikuwa ni Neno. Si ajabu Yeye angeweza kusimama pale na kuyapangusa machozi kutoka machoni Mwake, kama Mwanadamu; naye angeweza kuzungumza na mtu aliyekuwa amekufa, siku nne kaburini, na kusema, “Lazaro, njoo huku!” Hiyo ilikuwa ni nini? Hilo lilikuwa ni Neno. Amina! Hilo lilikuwa Neno katika matendo. Yeye alikuwa ni Neno. Hilo lilikuwa ni Neno lililowajia manabii. Hiyo ilikuwa, kila mmoja wa manabii alimtabiri Yeye.

128 Stefano kasema, kwa Baraza la wazee, “Ni nani kati ya baba zenu ambaye hakuwatesa wale waliomwona akija, waliomwona Mwenye Haki hapo awali, waliosema angekuja? Ni nani kati ya baba zenu ambaye hakumtesa? Sasa mmemchukua Mfalme wa Uzima, na mmemwua.” Loo, jamani! “Mlichukua Neno la Uzima, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Neno!”

129 Huyo hapo, Neno lilikuwa miongoni mwao. Walimwona akienda kwenye kaburi la wafu. Walimwona akimsimamisha yule mwanamke wa Naini kule chini, wakati msafara wa

mazishi, na mwanawe wa pekee, maiti, iliyotiwa dawa isioze, ikienda kaburini. Lakini hiyo maiti ikakutana na Neno. Ingawa ilikuwa maiti, hata hivyo akaishi!

¹³⁰ “Ajapokufa, hata hivyo ataishi.” Maiti ikafufuka, kwa sababu ilikutana na Neno. Loo, yale litakayofanya, wakati unapokutana na Neno hilo! Hiyo ndiyo faraja.

¹³¹ Loo, wakati mmoja, watu waliona hilo, kundi la Wagalilaya, labda wavuvi, nao walikuwa na maskini mzee mmoja aliyekuwa mgonjwa sana hata asingeweza kutoka kitandani mwake, nao wakajaribu kumpeleka kwenye Neno. Wala hawakuweza kupata nafasi, kwa kuwa kulikuwa na wengi walio na njaa kwa ajili ya Mungu. Nayo nyumba ilikuwa imejaa, kile kibanda kidogo, kibanda cha wavuvi huko chini mtoni. Walikuwa na vigae vichache kwenye paa. Na kumleta mtu huyu mbele ya Neno, hawakuwazia gharama ambayo ingewagharimu. Waliibomoa paa, chochote kile, kusudi tu waweze kukutana na Neno. Na mara Yeye, lile Neno, alipokiona kitanda kikija, kikishuka, Yeye alisema, “Umesamehewa dhambi zako, mwanangu. Jitwike kitanda chako, uende nyumbani.” Kwa nini? Alikuwa amekutana na Neno. Mnaona, yeye aliliamini.

Sasa, kama alikuwa amesema, “Lakini, unajua, nimekuwa hapa miaka hii yote, siwezi kufanya hivyo.” Lisingemfaa chochote.

¹³² Lakini wakati alipokutana na Neno, alilipokea Neno, akalipokea Neno kwa furaha. “Ninaamini Hilo. Ninajua ya kwamba ndivyo ilivyo. Ninajua Yeye ni Neno.” Kwa hiyo, mara tu alipokutana na Neno, alichukua kitanda chake akaenda zake.

Yule Farisayo akasema, “Mtu huyu anakufuru. Yeye anasamehe dhambi.”

Kasema, “Ni lipi lililo rahisi kusema, ‘Umesamehewa dhambi zako,’ au, ‘Jitwike godoro lako, uende?’” Uh-huh. Loo, jamani!

Walikosa kuona Yeye alikuwa ni Nani. Yeye alikuwa ni Neno.

Ni faraja jinsi gani kwa hao Wagalilaya! Jinsi walivyomwamini! Jinsi walivyompenda!

¹³³ Sasa, siku moja walimwona akienda Kalvari. Walimsikia akisema, “Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena.” Loo, “Mimi ni Mwana wa Adamu, sina budi kwenda Yerusalemu, na kuwekwa katika mikono ya watu wenye dhambi kusulubiwa, na nife.” Wangewezaje kulistahimili? Mioyo yao ilivunjika. Walikuwa wamefadhaika. Wao ni, wote walikuwa katika utusitusi. Wangewezaje kamwe kumwacha? Kwa sababu, lile Neno ambalo manabii walikuwa wamelinena, lile Neno ambalo wale wenye hekima, na watu wote wakuu watakatifu huko nyuma hata mwisho, mwanzoni mwa ulimwengu,

walikuwa wamenena juu ya Neno hilo, nalo Hili hapa miongoni mwao.

¹³⁴ Lakini basi, angalieni ahadi aliyotoa! “Sitawaacha ninyi yatima. Sitawaacha ninyi yatima. Nitamwomba Baba, Naye atawatumia Mfariji mwingine, ambaye ni Roho Mtakatifu, Naye atakaa nanyi milele; ndiye Roho wa Kweli, ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumjui Yeye. Haumwoni, wala haumtambui—kumtambua. Lakini mnamjua! Mnamjua kwa sababu Yeye yu pamoja nanyi, Naye atakuwa ndani yenu.”

¹³⁵ Hilo hapo! Naye atakaa muda gani? Milele! Basi Neno la Mungu ni nini? Faraja yetu ni nini leo? Ni wakati tunapopokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, na nguvu za Mungu aliye hai zikiishi ndani yetu. Na kwamba tukiwa na Neno la Mungu aliye hai, tunasimama, Neno hilo limefanyika mwili na kukaa miongoni mwetu. Sasa Neno lilo hilo, lililofanyika mwili na kukaa kwetu, limekuwa mwili wetu. “Yuko pamoja nanyi sasa, bali atakuwa ndani yenu.” Sasa Neno lilo hilo ambalo nabii alinena, Neno lilo hilo lililofanyika mwili, Neno lilo hilo linakaa Kanisani. Kwa hiyo, tusipopatana na Neno hilo, tunadumu moja kwa moja Nalo, tusipopatana Kwalo, Neno lilo hilo likiishi ndani yako litazaa kitu kile kile lililozaa wakati lilipofanyika mwili, kwa sababu mwili *wako* unaushikilia.

¹³⁶ Hiyo ndiyo sababu maono yanaweza kupenya kupitia kizuizi cha sauti. Hiyo ndiyo sababu ono linaweza kuvunja vizuizi vya wakati, na kusema, “BWANA ASEMA HIVI, itakuwa *hivi-na-hivi*.” Na hivyo ndivyo ilivyo. Ni kitu gani? Ni Neno likitoka kwa Roho.

¹³⁷ Hunioni mimi, unauona mwili wangu. Hunioni mimi. Sikuoni wewe, kwa sababu ninauona tu mwili wako. Huu ni mkono wangu, lakini mimi ninayeumiliki huo mkono ni nani? Huu ni mwili wangu, lakini mimi ni nani? Ni roho.

¹³⁸ Na kama nimezaliwa mara ya pili, kama umezaliwa mara ya pili, ni Roho Mtakatifu wa Mungu, Neno la Mungu linaloishi ndani yetu. Na kama tukipatana juu ya Neno hili, na kusema ya kwamba tuna Roho wa Mungu, tunawezaje kudai kuwa tuna Roho wa Mungu? Wakati Roho wa Mungu anaposhuhudia Neno Lake Mwenyewe; kamwe hatasogea hata inchi moja kutoka Kwake. Haidhuru madhehebu yanasema nini! Yeye ataondokaje Kwake, wakati ni Neno Lake Mwenyewe?

Ile ahadi, “Nitakuwa pamoja nanyi; yule Mfariji.” Alisema, “Nitamtuma Mfariji.”

¹³⁹ Nao wakakusanyika katika chumba cha juu, nao wakangojea mle mpaka Siku ya Pentekoste. Ndipo wakati Roho Mtakatifu alipokuja, sawasawa kabisa na Neno lilivyosema angefanya. Lilifanya yale hasa Mungu alisema lingefanya. Katika Isaya 28, ama 28:18, ama, naam, ninaamini ni Isaya 28:18 na 19. Ilisema, “Amri lazima iwe juu ya amri; kanuni

juu ya kanuni; hapa kidogo, na pale kidogo. Shikilia yaliyo mema. Kwa kuwa kwa midomo ya watu wageni na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa.” Hivyo ndivyo alivyosema angefanya. Paulo alilirejea, katika zile Nyaraka, “Kwa watu wa midomo mingine angesema na watu.” Basi wakati Roho Mtakatifu alipokuja, alikuja sawasawa kabisa na Neno.

¹⁴⁰ Utukufu! Basi atakapokuja tena, na anapoingia katika Kanisa lililozaliwa mara ya pili, atakuja pamoja na nguvu na dhahirisho la Utu Wake. Neno la Mungu, Mfariji ndani yetu, likileta jambo lenyewe hasa!

¹⁴¹ Hivi majuzi nilikuwa nikizungumza na kasisi fulani, akasema, “Mbona, wewe ni mwalimu tu wa Biblia.” Kasema, “Wewe, wewe dumu tu na Biblia.” Kasema, “Hiyo ni historia ya kanisa Katoliki.”

Nikasema, “Halafu leo mnadai kuwa wakuu zaidi?”

Akasema, “Hakika, tunabadilisha kile tunachotaka, unaona, maana inafanywa na ka—kanisa, mamlaka iliypewa kanisa.”

Nikasema, “Jambo fulani lilitukia! Kwa sababu, katika siku za mwanzoni, mlikuwa na ishara na maajabu na miujiza, kwamba Roho Mtakatifu alikuwa pamoja nanyi.”

¹⁴² Kanisa katoliki la mwanzoni lilinena kwa lugha. Kanisa katoliki la mwanzoni lilitabiri; walikuwa na manabii. Kanisa katoliki la mwanzoni lilifanya miujiza hii yote. Waliwaponya wagonjwa. Waliwafufua wafu. Walipiga mayowe, wakupiga makelele, walitenda kama wenye kichaa. Walicheza katika Roho. Waliitwa “wendawazimu.”

¹⁴³ Lakini mmekuwa wagumu sana siku hizi, ninyi Wakatoliki. Mnaona, mumeingia kwenye mtindo mpya. Wakati umewadia kwa kanisa Katoliki kurudi mahali lilipoanzia basi; hizo siku mlipotembea pamoja na Yesu wa Nazareti, naye Neno akafanyika mwili. Mnaona, mna kundi la makasisi na mapapa, na kadhalika mle ndani, ambayo yamelibadilisha Neno hilo na kulipotosha, wala hakuna nguvu tena kanisani. Ni madhehebu tu, kama vile Methodisti, Baptisti, Presbiteri, na Pentekoste, ni kitu kile kile; ni dhehebu. Hebu tuondoke kwenye dhehebu hili.

¹⁴⁴ Usijifungie kwenye vyumba vidogo vya gereza la dhehebu fulani, kama ghala lililo chini ya ardhi mahali fulani, ya kutokuamini, kulikana Neno la Mungu. Sijali yale askofu yeyote ama yeyote yule asemayo. Acha Neno liingie ndani yako, lililofanyika mwili kwa nguvu za Roho Mtakatifu, na kuchukua mamlaka juu ya mwili *wako* na kukutawala, kushuhudia kupitia kwako, kazi na nguvu kuu za Mungu aliye hai. Hiyo ni kweli. Haidhuru makanisa yalisema nini. Hayo madhehebu yanawaweka tu kwenye ghala lililo chini ya ardhi, nanyi mnajificha kutoka kwa mwanga wa Mwana uliobarikiwa. Ninajua hilo kuwa ni Kweli. Je, mnataka kukaa katika ghala la ardhini? Hakuna mtu anayefanya hivyo. Usiingie kwenye ghala

hilo la ardhini. Toka uingie katika mwanga wa Mwana! Toka ambapo, Neno, unaweza kulichukua Neno na kuliadini Neno, nalo Neno litajidhihirisha Lenyewe kwako, na kujidhihirisha Lenyewe kupitia kwako; kulidhihirisha Neno Lake, likifanya litimie!

¹⁴⁵ Kama tunamtarajia Mungu kutimiza Neno Lake, kama tukimtarajia Mungu kutufanyia mambo tunayoomba, kamwe hatutaweza kufanya hivyo mpaka tutakaporudi na kutii yale Mungu aliyosema tufanye. Hatuna budi kurudi mahali tulipoachia. Hatuna budi kurudi kwenye Pentekoste. Hatuna budi kurudi kwa yule Mfariji. Hatuna budi kumrudia Roho Mtakatifu, ambaye ndiye Faraja yetu. Ndipo Roho Mtakatifu ajapo, hatakana Neno lolote alilopata kusema. Atadumu moja kwa moja na hilo Neno, kwa kuwa ni Neno. Amina.

¹⁴⁶ Si ajabu maskini kipofu Fanny Crosby kamwe hakuwa ameona mapambazuko, walimwuliza ana mawazo gani juu ya Kristo, akasema:

Wewe uliye Kijito cha faraja yangu yote,
Zaidi ya maisha kwangu,
Ni nani niliye naye duniani ila Wewe?
Au ni nani Mbinguni ila Wewe?

Mfariji yupo hapa, Mfariji amekuja!
Ee enezeni habari kote, popote mwanadamu
apatikanapo:
Mfariji amekuja!

¹⁴⁷ Ni kitu gani? Neno la Mungu likitia nanga mwilini *mwako*, hilo linakupa Uzima wa Milele, hilo linakupa nguvu za ufufuo kukutoa katika mambo ya ulimwengu, kutoka kwa mapokeo yaliyopofuka ya mwanadamu, kutembea katika mwanga wa Mwana wa afya ya Mungu. Hivyo ndivyo Mfariji afanyavyo. Anakuinua kutoka kwenye hali hiyo ya kuwekwa kwenye ghala lililoko chini ya ardhi. Anakuinua juu Uweponi mwa Mungu, na kukupa tukio na Mungu, hata unaweza kupiga makelele pamoja na Ayubu, wa kale, "Ninajua Mkombozi wangu yu hai!"

¹⁴⁸ Basi, kama tukiliona Neno Lake, nasi tumekataa kutembea katika Nuru kama Yeye alivyo katika Nuru, basi ushirika wetu pamoja na Mungu umekatizwa. Lakini tunapoiona Nuru na kuenenda Nuruni, kama Yeye alivyo katika Nuru, basi twashirikiana sisi kwa sisi; na Damu Yake Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yatusafisha dhambi zote.

¹⁴⁹ Tunajiandaa, katika dakika chache, kuumeza mkate huo, mkate huo wa kosha ambao unawakilisha hilo Neno. Kamwe msisahau: Ile Faraja, kijito cha faraja yangu yote, kijito cha faraja yangu usiku wa leo, ni, ninajua ya kwamba Mungu hutimiza Neno Lake. Ninajua ya kwamba jambo fulani lilinipata. Ninajua ya kwamba nimepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Ninajua ya kwamba ninazishika Amri Zake. Kama

mimi. . . “Mkinipenda, zishikeni Amri Zangu,” Yeye alisema. “Mkinipenda Mimi, fanyeni yale ninayowaambia mfanye! Neno la kila mtu na liwe uongo; acha Langu liwe Kweli.” Usifuate yale mwanadamu aliyosema. Fuata yale Mungu aliyosema, na hapo unampata yule Mfariji. Nayo hiyo faraja inakuletea ridhaa, ya kujua, ni BWANA ASEMA HIVI.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

¹⁵⁰ Yehova mkuu, Mwenye Nguvu! Kama vile Fanny Crosby, nilivyonukuu dakika chache zilizopita, alivyosema, “Wewe, Kijito cha faraja yangu yote!” Hakika, Bwana, ninaungana naye usiku wa leo, pamoja na kanisa hili dogo, katika kusema, “Wewe, Kijito cha faraja yangu yote!”

Ninashikilia, chini ya mkono wangu, lesa kutoka kwa wagonjwa, Bwana. Zinawaandaa wanaoteseka. Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utawaponya.

¹⁵¹ Wewe ni Neno. Nalo Neno linakuja miongoni mwetu, Neno linakaa ndani yetu. “Sitawaacha ninyi yatima. Nitakuja tena. Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa ndani yenu hata ukamilifu wa dahari.” Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya jambo hilo, Bwana!

¹⁵² Kuona nguvu Zako zikishuka moja kwa moja katika maisha ya—ya mwenye dhambi, zikaingia ndani ya mwanamke mnyonge, msichana aliyevuka mipaka ya uadilifu, akatoka kwenye uadilifu akawa mtovu wa uadilifu; mvulana aliyetoka kwenye uadilifu, akaingia kwenye jukwaa la ulevi, la kuvuta sigara; kwa mwanamke aliyejifanya mtovu wa uadilifu kwa pepo, ambaye amevaa maskini nguo chafu, apate kujianika mbele ya wanaume: Kumwona mwanamke huyo akiinuka akaingia kwenye umama wenye heshima! Kumwona mvulana huyo akiweka kando hizo sigara na unywaji pombe, akijongea mbele na kuwa mtakatifu wa Mungu, mhubiri mimbarani! Bwana Mungu, tunajua nguvu Zako kuu zinaweza kufanya mambo yote. Kuona kile kivuli cha mtu aliyelala pale, ameliwa na kansa, akifa; yule kipofu aliyesimama kule; kuwaona wakifufuka na kuishi! Loo, hilo Neno la Mungu aliye hai! Jinsi tunavyokushukuru, Bwana!

Wewe ndiwe Kijito cha faraja yetu yote. Nina furaha sana, usiku wa leo, kwamba Mfariji amekuja na ahadi, “Nitakaa pamoja nanyi milele.”

¹⁵³ Na yule mtume mashuhuri aliyepewa funguo za Ufalme, alisema, kwenye Siku hiyo ya Pentekoste, “Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjije.” Basi, tunajua ya kwamba Mfariji yuyo huyo anakuja. Nasi tunajua ya kwamba Yeye ni Mwokozi wetu, usiku wa leo, kwa sababu Yeye hujionyesha Mwenyewe miongoni mwetu, kama

alivyofanya wakati huo. Hivyo ndivyo tunavyomjua Yeye, kwa sababu Yeye huamini na kutekeleza kila Neno alilopata kunena. Hawezi kulighairi, kwa sababu Yeye ni Mungu. Tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili, Baba.

¹⁵⁴ Nami ninaomba ya kwamba Wewe utaufariji kila moyo hapa, usiku wa leo. Wafariji watu hao. Wape Roho Wako. Waponye wagonjwa na wanaoteseka. Loo, mchukue mwanamke huyo aliyefadhaika, mwanamume huyo aliyefadhaika, mvulana au msichana, na jalia waangalie mbali usiku wa leo, kutoka kwenye dhambi zao, jalia waangalie mbali na mambo ya ulimwengu, wamtazame Yesu aliyeahidi ya kwamba atakaa ndani yetu. Na kazi alizofanya, sisi nasi tungezifanya, kwa sababu Yeye angekuja katika umbo la Roho Mtakatifu, kuwa Mfariji adumuye, awe pamoja nasi milele. Baba, tujalie baraka hizo. Waponye wagonjwa, tena naomba, Baba. Wengi wao wanateseka na ni wahitaji.

¹⁵⁵ Sasa tunakuja kwenye meza ya ushirika, kuchukua vifurushi hivyo tulivyoachiwa, agizo, “Fanyeni hivi mpaka atakaporudi.” Tunashukuru kwa ajili ya mambo haya, Baba. Nasi tunaomba hilo katika Jina la Yesu, ya kwamba kama kuna mtu mnyonge miongoni mwetu usiku wa leo, anayekuja kwenye meza hii ya ushirika . . .

¹⁵⁶ Bwana, ninaweza tu kumwona yule mama yangu mzee anayetemeka akitembea kwenye marefu ya kanisa pale, mara ya mwisho alipokuwa hapa kula ushirika huo, jinsi maskini mikono yake iliyokuwa ikitetemeka ilivyotetemeka kwenye sahani hiyo. Nilisimama hapa na kumwangualia, huku machozi yakidondoka moyoni mwangu. Lakini huyo hapo amelala usiku wa leo, akitazama Kalvari. Ee Mungu, jinsi ninavyoshukuru! Wewe ulisema, “Aulaye mwili Wangu na kuinywa Damu Yangu, yuna Uzima wa Milele. Nami nitamfufua tena katika siku ya mwisho.”

Bwana, hilo ndilo Neno. Hiyo ndiyo sababu ninaweza kusimama na kusema, “Ninamwamini Mungu!”

¹⁵⁷ Sasa, Baba, tunatambua ya kwamba wakati hili lilipoamriwa kwanza, huko nyuma nyikani, na huko nyuma Misri, yule mwana-kondoo wa pasaka alichinjwa. Walisafiri miaka arobaini, na hapakuwapo na mnyonge miongoni mwa wale milioni mbili waliotoka. Uliwadumisha katika afya wakati walipokula Pasaka. Ee Mungu, mponye kila mgonjwa anayejitokeza. Tujalie, Bwana. Mwokoe kila mwenye dhambi. Na umjaze kila mwaminio na Roho Mtakatifu. Na jalia Mfariji akae mpaka atakapofanyika mwili miongoni mwetu katika Utu wa Yesu Kristo tena. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza

Na kununua wokovu wangu
Juu. . .

158 Mnampenda? Hebu tufunge macho yetu, tuinue mikono yetu na tuuimbe huo kutoka moyoni mwetu.

Na- . . . na- . . .
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

159 Sasa kuna askari msafiri anayeketi karibu nawe, ndugu au dada fulani aliye safarini. Wanasafiri njia ile ile unayopitia. Wanampenda Yeye unayempenda. Tunapoimba huu, *Nampenda*, na iwe ni ushuhuda. Peana tu mikonono na mtu fulani, karibu nawe, namna hiyo. Sasa wakati tukiuimba tena, katika kuabudu tu, mwajua. Ninapenda tu jambo hili, baada ya Ujumbe. Paulo alisema, “Nikiimba, nitaimba katika Roho.” Peana tu mkono na mtu fulani, nyosha mkono na kusema, “Mungu akubariki.”

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Nampenda . . .

Uimbeni katika Roho sasa!

. . . Nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

160 Sote pamoja sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa:

Baba yetu uliye Mbinguni, Jina Lako
Litukuzwe.

Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yafanyike
duniani, kama huko Mbinguni.

Utupe leo riziki yetu ya kila siku.

Na utusamehe makosa yetu, kama sisi nasi
tuwasameheavyo wanaotukosea.

Na usitutie majaribuni, bali utuokoe na yule
mwovu; kwa kuwa Ufalme ni Wako, na
nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.

161 Ee Mungu wa Milele, Mwanzilishi wa uzima na Mpaji wa vipawa vyote vyema, itakase mioyo yetu michafu, Bwana. Jalia Malaika atoke madhabahuni, akiwa na makoleo na kaa la moto, na kugusa midomo yetu na mioyo yetu, na kutakasa mawazo yetu na nia zetu, na nafsi zetu; ili kwamba tunapokula mkate huu wa kosha, tufanye hivyo kwa ukumbusho wa Bwana wetu. Kwa maana imeandikwa, “Alaye na kunywa isivyostahili, yuna hatia.” Ee Mungu, jalia tusihukumiwe pamoja na ulimwengu, lakini jalia tutakaswe na kutengwa na ulimwengu, tupate

kuwa Nuru zinazoangaza, kama Neno la Mungu likidhihirishwa maishani mwetu. Tutumie, kama watumishi Wako, Bwana. Tutumie, sote pamoja. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁶² Sasa, kwa wale ambao huenda ikawabidi kuondoka, na wana masafa marefu ya kuendesha gari, tutawaruhusu mwondoke. Ndipo tutaenda moja kwa moja kwenye ushirika, mara moja, kwa wale ambao wangetaka kukaa na kula ushirika pamoja nasi. Lakini kama inakubidi kwenda . . . Ninajua ni sasa, kwa saa yangu, saa nne kasoro dakika ishirini na tano. Labda itakuwa saa nne kamili kabla hatujamaliza ushirika. Halafu basi, mara baadaye, watatawadhha miguu. Na kama ungetaka kukaa na kuadhimisha hili pamoja nasi, tungefurahia sana kuwa pamoja nawe. Asanteni tena, kwa yote mliyomaanisha kwa Ufalme wa Mungu, na kwangu mimi na kwa walio wangu. Mungu awe nanyi daima!

¹⁶³ Ninataka kumshukuru maskini yule kaoboi, asubuhi ya leo, jamaa mdogo karibu *hivyo*, aliyevaa maskini kofia ya kaoboi, alikuja kule akanipa pochi, pochi ndogo iliyoandikwa jina langu, “Kasisi William Branham,” na zawadi ndogo. Sijui huyo mvulana mdogo ni nani. Nilikuwa nimehangaika sana, asubuhi ya leo, hata nikasahau kumshukuru maskini jamaa huyo. Lakini nakushukuru, kipenzi.

¹⁶⁴ Naye Billy alisema ya kwamba watu wengi hapa walimletea zawadi ndogo, apate kunipa mimi. Billy atafanya hivyo. Kwa hiyo, asanteni, sana. Mungu daima awabariki sana! Kumbukeni hili, “Kadiri mliyomtendea aliye mdogo sana wa hawa, watoto Wangu, mmenitendea Mimi.”

¹⁶⁵ Mungu awabariki daima, ndilo ombi langu. Na kama inawabidi kuondoka sasa, vema, tunawatakia yaliyo mema sana ya Mungu. Na kama mnaweza kukaa pamoja nasi, tutafurahia kuwa pamoja nanyi.

¹⁶⁶ Sasa, tutasimama, na kuimba ubeti mmoja wa *Peleka Jina la Yesu*. Ndipo, wale wanaopaswa kuondoka wataruhusiwa kwa maombi, mara baadaye.

Peleka Jina la Yesu,
Mtoto wa huzuni na sikitiko;
Litakupa furaha na faraja,
Lipeleke kila uendako.

Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha za Mbinguni.

¹⁶⁷ Tutaimba ubeti mmoja zaidi, kisha nitamwomba maskini mhudumu, ninaamini yeye ni Myunani, ambaye nilikutana naye wakati fulani uliopita. Siwezi kukumbuka jina lake sasa hivi. Ndugu Mamalis. Yeye amesimama pamoja nasi, hapa pamoja

nasi usiku wa leo. Tuna furaha kuwa naye. Ninaamini yeye ni mwanafunzi wa chuo fulani. Ninaamini nilikutana naye hapa si muda mrefu uliopita, ndugu mwaminifu kweli akijaribu kutimiza wokovu wake kwa hofu na kutetemeka. Anatoka Uyunani. Anazungumza lugha hiyo kwa ufasaha. Na kwa hiyo tuna furaha kuwa na ndugu pamoja nasi usiku wa leo. Ninaamini unatoka huko mbali Oregon, ama, California, ama, Los Angeles. Tuna furaha kuwa pamoja naye.

¹⁶⁸ Sasa, tutaimba ubeti mmoja zaidi, tumpe nafasi ya kujituliza. Ndipo ataturuhusu tufumukane kwa maombi, tafadhali, ndugu yangu. Vema.

Kwa kulisujudia Jina la Yesu,
Kuanguka kifudifudi miguuni Pake,
Mfalme wa wafalme Mbinguni tutamvika taji,
Safari yetu itakapokamilika. (Hilo si litakuwa zuri sana?)

Jina la thamani, (Jina la thamani!) Loo jinsi lilivyo tamu!

Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
La thamani . . . Ee jinsi lilivyo tamu!

Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa. Vema, ndugu.

¹⁶⁹ [Ndugu Mamalis anaomba—Mh.] Naam. Kweli. Naam, Bwana. Naam. Tujalie. Naam. Tujalie, Bwana. Naam. Tujalie. Naam. Naam, Baba. Fanya, Baba. Naam, Kristo. Tujalie, Bwana. Naam. Naam, tujalie. Naam, Bwana. Amina.

¹⁷⁰ Kwenu, sasa, mnaolazimika kuondoka, nendeni sasa . . . ninyi ambao mngeruhusiwa kuondoka; na ninyi mnaotaka kubaki kwa ajili ya ushirika ketini tu.

Kwa kulisujudia Jina la Yesu,
Kuanguka kifudifudi miguuni Pake,
Mfalme wa wafalme . . . Yeye,
Wakati safari yetu . . . (Tupe pambio hilo tena.)

Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!

Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;

Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!

Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Amani! Amani! Amani ya ajabu,
Ukishuka kutoka kwa Baba aliye Juu;
Pitia kwenye roho yangu milele, naomba,
Katika mawimbi yasiyopimika ya upendo.

Amani! Amani! Amani ya ajabu,
Ikishuka kutoka kwa Baba aliye Juu;
Pitia juu ya roho yangu milele, naomba,
Katika mawimbi yasiyopimika ya upendo.

Kuwa kama Yesu, kuwa kama Yesu,

Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
Kote katika safari ya maisha kutoka duniani
hadi Utukufuni
Ninaomba tu kuwa kama Yeye.

Kutoka kweye hori la Bethlehemu alitokea
mgeni,
Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
Kote katika safari ya maisha kutoka duniani
hadi Utukufuni
Ninaomba tu kuwa kama Yeye.

Niangazie, Bwana, niangazie,
Hebu Nuru kutoka kwenye Mnara wa taa
iniangazie;
Loo, niangazie, Bwana, niangazie,
Hebu Nuru kutoka kwenye Mnara wa taa
iniangazie.

Hebu tuinue mikono yetu tunapouimba huo.

Niangazie, loo, Bwana, niangazie... (Huo ni
Uzima wa Roho, huo ni Uzima wa Roho.)
Hebu Nuru kutoka kwenye Mnara wa taa
iniangazie...
Loo, niangazie... Bwana, niangazie,
Hebu Nuru kutoka kwenye Mnara wa taa
iangaze... .

Kuwa kama Yesu, kuwa kama Yesu,
Duniani natamani kuwa (...?...) .
...katika safari ya maisha kutoka duniani
hadi Utukufuni
Ninaomba tu kuwa kama Yeye.

Ee Mungu!

Tutatembea Nuruni, Nuru nzuri,
Inakuja ambapo umande wa rehema unang'aa;
Angaza kote kutuzunguka mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Njoni enyi watakatifu wote wa Nuru
tangazeni,
Yesu, Nuru ya ulimwengu;
Ndipo kengele za Mbinguni zitalia,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Tutatembea katika Nuru hii, ni Nuru nzuri
sana,
Inakuja ambapo matone ya umande wa rehema
yanang'aa;
Angaza kutuzunguka mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

¹⁷¹ Baba, tunakushukuru kwa ajili ya nyimbo hizi. Tunaamini ya kwamba hizo ni unabii. Tunawazia jinsi Yesu, wakati alipokuwa hapa duniani, alirejea kwenye Zaburi. Akasema, “Je, Daudi hakusema katika Zaburi, *hivi-na-hivi?*” Ule uvuvio wa mwandishi.

¹⁷² Loo, tunapowazia juu ya wimbo huu, *Tutatemba Nuruni*, ama *Kuwa Kama Yesu* na jinsi tunavyoupenda huo, kwa sababu hayo ndiyo matarajio yetu makuu. Ni nia na kusudi letu. Ni shauku ya maisha yetu kuwa kama Yeye. Halafu katika kumalizia kwa mwisho tunawazia juu ya wimbo unaoimbwa hivi:

Kutakuwa na mkutano hewani,
Katika utamu huo, utamu hivi karibuni.

Loo, jinsi tunavyoupenda. Na mshairi aliposema:

Mmesikia habari za maskini Musa kwenye
kichaka,
Pia mmesikia habari za Daudi shujaa na
kombeo lake;
Mmesikia hadithi ikisimuliwa ya Yusufu
aliyeota ndoto,
Na juu ya Danieli na simba sisi mara nyingi
tunaimba.
Loo, kuna wengine wengi, wengi sana katika
Biblia,
Nami ninatamani kukutana nao wote,
ninatangaza!
Karibuni sana Bwana atatujalia kukutana nao
Kwenye mkutano huo hewani.

¹⁷³ Lakini tunapofikia mahali hapo ambapo unasema, “Lakini Mwana wa Mungu Mwenyewe atakuwa Ndiye anayeongoza kwenye mkutano huo hewani,” tunatamani jambo hilo, Bwana. Tunakuabudu sasa. Kwa mioyo yetu yote, tunakuabudu, “Wewe Kijito cha faraja yetu yote.”

¹⁷⁴ Milango ya mioyo yetu imefungwa kwa ulimwengu wa nje, tunaelekea sasa kwenye meza ya ushirika. Tunaweza kumsikia Bwana wetu akimwambia Petro usiku huo, “Nisipokuosha, huna shirika nami.”

¹⁷⁵ Akasema, “Bwana, si miguu yangu tu, bali na mikono yangu na kichwa changu.” Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya utaratibu huu, Bwana, kwamba tunaweza kushiriki pamoja. Itakase mioyo yetu sasa, Bwana, kama kuna dhambi miongoni mwetu, iondoe, Baba.

¹⁷⁶ Utusamehe makosa yetu, nasi huwasamehe wengine wanaotukosea. Ulihidi, Bwana, ya kwamba kama tukiwasamehe wengine, ya kwamba Wewe ungetusamehe. Na Baba, kutoka kwenye kilindi cha moyo wangu, ninamsamehe kila adui. Loo, Mungu. Ningeweza kuwaendea, vizuri moyoni

mwangu, na kuosha miguu yao, nifanye chochote ambacho ningeweza, kusudi tu wasiukose utamu huo mtukufu hivi karibuni. Nami ninajisikia ya kwamba hiyo ndiyo hisia ya kila moyo hapa ndani sasa, Baba.

¹⁷⁷ Tumekusanyika pamoja, milango imefungwa, mapazia yamevutwa chini na sasa tunakuja kwenye meza hii takatifu. Na tunaposoma utaratibu huu, tunaomba Roho Mtakatifu atabariki, aokoe na kumponya kila mtu katika Uwepo wa Kiungu. Tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.

¹⁷⁸ Muda mfupi tu uliopita, nilipofungua Biblia yangu hapa kusoma, kutafuta Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 11 na kifungu cha 23, ilifunguka tu moja kwa moja hapo. Nitasoma sasa kutoka kwenye maandiko ya huyu mtume mashuhuri kwa Wakorintho:

Kwa maana mimi nimepokea kwa Bwana... niliyowapa ninyi, Ya kuwa Bwana Yesu usiku ule... aliosalitiwa alitwaa mkate:

Naye akiisha...kushukuru, akaumega, akasema, Twaeni, mle: huu ndio mwili wangu, uliovunjwa kwa ajili yenu: fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.

Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu: fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu.

Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.

Basi kila aulaye mkate huu, au kukinywea kikombe hiki... , isivyostahili, atakuwa na hatia ya mwili na damu ya Bwana.

Lakini mtu na ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe.

Maana alaye na kunywa isivyostahili, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili wa Bwana.

Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio wagonjwa, ama—ama, wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaidu, na watu kadha wa kadha wamelala.

Lakini kama...tungejipambanua...Lakini kama tugejiipambanua nafsi zetu, tusingehukumwiwa—tusingehukumwiwa.

Ila tuhukumwiwapo, twarudiwa na Bwana, isije ikatupata adhabu pamoja na dunia.

Kwa hiyo, ndugu zangu, mkutanikapo mpate kula, mngojaneni.

¹⁷⁹ Sasa, imekuwa ni desturi ya kanisa letu kwamba tunapofikia wakati huu, tunainama kwa muda kidogo tu katika maombi; nanyi mniombe, kimyakimya, ninapowaombea.

¹⁸⁰ Tunatambua ya kwamba Maandiko ambayo tumesoma, ya kwamba, tukila na kuinywa isivyostahili, tunakula na kunywa hukumu ya nafsi zetu, kwa kutokuupambanua mwili wa Bwana. Hiyo ni kusema: kama unaishi katika dhambi, ukiishi mahali ambapo hupaswi kuishi, basi wewe ni fedheha kwa huduma. Usiule, kaa mbali nao. Usifanye hivyo.

¹⁸¹ Lakini kama unaishi . . . Ninajua kila mmoja wetu hukosea, bali tuna Dhabihu ya Damu iliyowekwa pale ikifanya upatanisho kwa ajili yetu sikuzote, Damu ya Mwana wa Mungu Mwenyewe. Kwa hiyo tumesamehewa dhambi zetu.

Lakini kama unaishi katika dhambi iliyo dhahiri na hu—hustahili kuitwa Mkristo, usiule.

¹⁸² Lakini kama wewe ni Mkristo, basi unawajibika kuula. “Kwa maana aulaye mwili Wangu na kuinywa Damu Yangu yuna Uzima wa milele, nami nitamfufua katika siku ya mwisho.”

¹⁸³ Na tuombeane, kwa muda kidogo tu, mmoja kwa mwingine.

Baba, ombi hili tunakutolea Wewe, msamaha wa dhambi zetu, tunaomba, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mabawabu kwa kawaida huwafanya watu kusimama kwenye . . . Yuko wapi Ndugu Taylor na hao wengine? Vema. [Ndugu Branham anatulia—Mh.]

¹⁸⁴ Kama kawaida, ninaomba sala hii kabla mtu yeyote hajasimama. Hiyo ndiyo sababu Ndugu Taylor alikuwa akingojea, bali nilitaka jambo hili kwa sababu fulani usiku wa leo. Ninashika mkononi mwangu maji ya zabibu, divai, damu ya zabibu ambayo Yesu alisema, “Nitainywa upya pamoja nanyi katika Ufalme wa Baba Yangu.” Hii inawakilisha Damu ya Yesu Kristo, kwamba dhambi zetu zimesamehewa.

¹⁸⁵ Ninawazia juu ya yule mshairi aliyesema, “Mwana-Kondoo mpendwa anayekufa, Damu Yako ya thamani kamwe haitapoteza nguvu Zake mpaka Kanisa lote la Mungu lililokombolewa litakapokolewa lisitende dhambi tena.” Na tuinamishe vichwa vyetu.

¹⁸⁶ Mungu mwenye rehema, ninaposhikilia, katika huu, mkono wangu, usiku wa leo, zabibu, damu ya zabibu, hiyo ni kuwakilisha Damu ya Mwana wa Mungu. Mara nyingi nimewazia, “Ningefanyaje na matone mawili ya Damu halisi ya Yesu, kama ningalikuwa nayo katika bilauri?” Jinsi ningeisukumia moyoni mwangu. Sasa, Baba, hii ni kuiwakilisha ile Damu.

¹⁸⁷ Ninapokuomba uibariki kwa kila mshiriki, jalia dhambi zetu ziwe chini ya Damu. Jalia ugonjwa wetu utoweke kwetu, kwa kuwa sisi ni watumishi Wako tukiwa na shauku ya miili yenye

nguvu, yenye afya na safi, moyo safi na dhamiri, ili tuweze kuwa wawakilishi Wako katika dunia hii. Tunakuomba Wewe, Mungu wetu, utakase zabibu hizi usiku wa leo, damu ya zabibu hii, kwa kusudi lililokusudiwa, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

¹⁸⁸ Maandiko yanasema ya kwamba Yeye alikitwaa kikombe na kushukuru. Kisha akachukua mkate na akaumega na kusema, “Huu ni mwili Wangu uliovunjwa kwa ajili yenu.” Ninaposhika mkononi mwangu, usiku wa leo, maskini vifurushi hivi vya mikate ambavyo vimekunjamana na kuvunjika, inanikumbusha juu ya ule ujumbe usiku wa leo, jinsi walivyopiga mti mmoja wapate nyama yake kuuokoa huo mwingine, na jinsi ambavyo “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kuchubuliwa kwa maovu yetu: adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; bali kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Jalia neema ya Mungu itakase mkate huu wa kosha kwa kusudi lake lililokusudiwa, na kila mtu anayeushiriki, hakuna dhambi tena maishani mwako, hakuna ugonjwa tena mwilini mwako mpaka tutakapokutana na Bwana.

¹⁸⁹ Baba yetu wa Mbinguni, tunautakasa mkate huu kwa neno la maombi na imani kwamba utatumiwa kwa kusudi lililokusudiwa ambalo Mungu amekusudia tufanye: kudumisha utaratibu huu mpaka atakapokuja. Jalia kila mtu anayeshiriki chakula hiki cha jioni usiku wa leo, na awe safi kutokana na dhambi, na kuponywa kutokana na maradhi, kwa ajili ya safari iliyo mbele yetu. Tunaomba, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

¹⁹⁰ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]... asubuhi. [Ndugu Branham anasoma kutoka Yohana 13:2-15.]

... chakula cha jioni kilipokuwa kimekwisha, ibilisi sasa amekwisha kumtia Yuda Iskariote, mwana wa Simoni, moyo wa kumsaliti;

Yesu hali akijua ya kuwa Baba amempa vyote mikononi mwake, ... ya kuwa alitoka kwa Mungu, naye anakwenda kwa Mungu;

Aliondoka chakulani, akaweka kando mavazi yake; ... akatwaa kitambaa, akajifunga kiunoni.

Kisha akatia maji katika bakuli, akaanza kuwatawadha wanafunzi miguu, na kuipangusa kwa kile kitambaa alichojifunga.

Hivyo yuaja kwa Simoni Petro: ... Petro akamwambia, Bwana, wewe wanitawadha miguu mimi?

Yesu akajibu, akamwambia, Nifanyalo wewe hujui sasa. . . ; lakini utafhamu baadaye.

Petro akamwambia, Bwana, wewe hutanitawadha miguu kamwe. Yesu akamwambia, Kama nisipokutawadha, huna shirika nami.

Simoni Petro akamwambia, Bwana, si miguu yangu tu, hata na mikono yangu na kichwa changu pia.

Yesu akamwambia, Yeye aliyekwisha kuoga hana haja ila kutawadha miguu, bali yu safi mwili wote: nanyi mmekuwa safi, lakini si nyote.

Kwa maana alimjua yeye atakayemsaliti; ndiyo maana alisema, Si nyote mlilo safi.

Basi akiisha kuwatawadha miguu, na kuyatwaa mavazi yake, na kuketi tena, akawaambia, Je, mmeelewa na yale niliyowatendea?

Ninyi mwaniita Mwalimu na Bwana: nanyi mwanena vema; maana ndivyo nilivyo.

Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu; inawapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi.

Kwa kuwa nimewapa kielelezo, ili nanyi mtende kama nilivyowatendea.


“Na hivyo imetupasa kutimiza haki yote.”

Wanawake watawadhe miguu huko nyuma, naamini, chumbani upande wa kulia. Wanaume waingie kwenye chumba hiki hapa.

¹⁹¹ Na bila shaka mmealikwa na kwa moyo mkunjufu kukaa pamoja nasi kwa ajili ya jambo hili kama mkiweza. Kama hamwezi, mbona, tuna furaha kuwa tumekuwa nanyi hapa usiku wa leo; tunaomba ya kwamba mtarudi pamoja nasi tena, muwe pamoja nasi kwenye ibada yetu ijayo.

¹⁹² Ninataka kusema jambo moja, kila usiku ninapokula ushirika, daima ninararua kabisa, nikihubiri kwa nguvu. Lakini hakika inasisimua nafsi yangu kuona kundi la wanawake wanaoonekana safi kama wetu wakija kwenye maskani hii, wakija kwenye madhabahu hii hapa wakiwa na nyuso zilizooshwa, bila vipodozi, nywele ndefu, wamesimama pale kama watakatifu pamoja na wanawake waliovalia vizuri.

¹⁹³ Kuwaona ndugu zetu wakitembea pale na huo uso mkali, mtakatifu, wapate kula ushirika. Nina furaha kuwa mmoja wa wachungaji wenu. “Mungu awabariki daima,” ndilo ombi langu.

¹⁹⁴ Sasa, Ndugu Neville ataliruhusu kusanyiko liondoke wale ambao hawana budi kwenda. Na hao wanaume wanaotaka kuja na kutawadha miguu watakuja kwenye chumba upande wa kulia, nao wanawake wataenda kwenye chumba huko nyuma. Mpaka nitakapowaona tena, baraka za Mungu ziwe pamoja nanyi. Ndugu Neville. 

61-1001E Yule Mfariji
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org